USAWIRI WA MHUSIKA PADRI KATIKA RIWAYA ZA KEZILAHABI

Uchunguzi katika *Rosa Mistika*, *Gamba la Nyoka* na *Nagona*

Peres Gregory Mosha

Tasinifu ya M.A. (Kiswahili)
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Oktoba, 2013

USAWIRI WA MHUSIKA PADRI KATIKA RIWAYA ZA KEZILAHABI

Uchunguzi katika *Rosa Mistika*, *Gamba la Nyoka* na *Nagona*

Na

Peres Gregory Mosha

Tasinifu iliyowasilishwa kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digirii ya M. A (Kiswahili) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Oktoba, 2013

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba amesoma tasinifu hii "**USAWIRI WA MHUSIKA PADRI KATIKA RIWAYA ZA KEZILAHABI: Uchunguzi katika *Rosa Mistika, Gamba la Nyoka* na *Nagona"*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kwa minajili ya kukamilisha masharti ya Digirii ya M.A. (Kiswahili) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Dkt. A. K. Mutembei

(Msimamizi)

Tarehe: ----------

IKIRARI

NA

HAKIMILIKI

Mimi, **Peres Gregory Mosha,** nathibitisha kwamba, tasinifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Digrii kama hii au Digrii nyingine yoyote.

.....

Saini

.....

Tarehe

Haki ya kunakili tasinifu hii inalindwa na Mkataba wa Berne, Sheria ya Haki ya Kunakili ya mwaka 1999 na Mikataba mingine ya kitaifa na kimataifa inayolinda mali za kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili au kutafsiri kwa njia yoyote ile au kwa mfumo wowote ule ama iwe ni yote au sehemu ya tasinifu hii bila ya idhini ya maandishi kutoka ofisi ya Kurugenzi ya Masomo ya Uzamili kwa niaba ya mwandishi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kinachoruhusiwa ni madondoo mafupi mafupi kwa makubaliano halali kwa ajili ya tafiti, tahakiki au mijadala ya kitaaluma.

SHUKRANI

Kwa hakika si kazi rahisi kuwataja na kuwashukuru kwa majina wote waliochangia kukamilika kwa utafiti huu. Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote ambao wamewezesha kukamilika kwa utafiti huu. Wafuatao wanastahili shukrani za pekee.

Kwanza, namshukuru msimamizi wangu Dkt. A. K. Mutembei kwa kukubali kunisimamia na kuhakikisha kuwa ninaukamilisha utafiti huu. Kwa hakika mawazo yake na ushauri wake vimekuwa na msaada mkubwa sana kwangu katika kuukamilisha utafiti huu.

Pili, Naushukuru uongozi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mwenge, na kwa kipekee Mkuu wa Chuo Dkt. Filbert Vumilia kwa kukubali kufadhili masomo yangu katika kiwango cha shahada ya umahiri katika Kiswahili.

Tatu, ninapenda kuwashukuru wahadhiri wote katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) walionifundisha na kutoa muda wao wa thamani kunishauri na kunielekeza. Kipekee namshukuru Prof. M.M. Mulokozi kwa kupitia wazo la utafiti na kulifanyia marekebisho pamoja na kutoa maoni yake pale alipoona yafaa. Hakika mawazo yake yalinipa ari ya kuendelea na utafiti huu katika ngazi ya pili ya pendekezo la utafiti.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru wanafunzi wenzangu wote wa Digrii ya M.A. Kiswahili kwa mwaka wa masomo 2011/2012. Kipekee niwashukuru Aneth Kasebele, Jubeck Masebo, Nsia Kweka, Martha Mageni na Scolastica M. John.

TABARUKU

Naitabaruku tasinifu hii kwanza, **kwa watoto yatima wote duniani**. Mungu ni baba yenu. Pili, kwa **wote wanaopitia hali ngumu**. Kumbukeni kuwa mkiisha kupitia hali ngumu mtakuwa wagumu na hatimaye hali ngumu zitawaogopa kwa sababu ya ugumu wenu na zitawakimbia. Tatu kwa **watoto wangu wapenzi Holiness Peres na Faith Peres** kwa uvumilivu wao kwa kipindi chote nilichokuwa masomoni. Ninyi ni nguvu zangu.

IKISIRI

Utafiti huu unahusu usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi; uchunguzi unaofanyika katika *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990). Utafiti huu ulijikita katika malengo makuu matatu. Mosi, kuchambua uhusika wa mhusika Padri katika riwaya teule, pili, kujadili dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya teule, na tatu, kubainisha motifu inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya teule. Mtafiti alifuatilia hatua kwa hatua matendo ya mhusika Padri, maneno yake na yale ambayo wahusika wengine wanasema kumhusu. Kupitia mambo haya ilibainika kuwa mhusika Padri anasawiriwa katika nafasi mbalimbali kama vile: Padri kama kiongozi wa Kanisa katika jamii ambapo ana jukumu la malezi ya kiroho na kufanya shughuli za ibada, Padri kama mwanamume wa kawaida katika jamii ambapo anaonekana katika matendo kama vile uzinzi, ulevi, ugomvi na kadhalika. Pia tumeona kuwa mhusika Padri anatokea kama mtu mwenye sauti katika jamii na kama mwelekezaji. Utafiti huu pia ulibaini kuwa mhusika Padri katika riwaya teule za Kezilahabi anawasilisha dhamira kuu nne ambazo ni suala la malezi ya kiroho, unafiki wa viongozi wa Kanisa Katoliki, Uonevu na kukosekana haki na suala la uwezo wa Padri kuondoa dhambi. Kwa kutumia nadharia ya uhalisia wa Kimarx tuliona kwa mifano mbalimbali kwamba matendo yanayojadiliwa katika riwaya za Kezilahabi kupitia mhusika Padri ni halisi katika jamii. Aidha tumebaini kwamba motifu ya Padri aliyeshindwa inajitokeza katika riwaya teule za Kezilahabi. Hii ni aina mpya ya motifu katika fasihi ya Kiswahili. Tumebaini pia kuwa mhusika Padri si mhusika wa kawaida bali ni mhusika wa kimotifu (mhusika anayewakilisha motifu).

YALIYOMO

Uthibitisho..... ii

Ikirari na Hakimiliki iii

Shukrani iv

Tabaruku.... v

Ikisiri..... vi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA UTAFITI 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli 1

1.3 Tatizo la Utafiti 3

1.4 Malengo ya Utafiti 5

1.5 Maswali ya Utafiti 6

1.6 Umuhimu wa Utafiti 6

1.7 Mawanda ya Utafiti 7

1.8 Hitimisho 7

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA 9

2.1 Utangulizi 9

2.2 Tafiti Tangulizi na Mapitio ya Maandiko 9

2.3 Kiunzi cha Nadharia 16

2.4 Hitimisho 18

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI..... 19

3.1 Utangulizi.....19

3.2 Mbinu za Ukusanyaji Data.....19

3.3 Sampuli na Usampulishaji 21

3.4 Uchambuzi, Uchakataji na Uwasilishaji wa Data.....22

3.5 Vifaa vya Utafiti.....23

3.6 Eneo la Utafiti 23

3.7 Hitimisho.....24

SURA YA NNE: UCHAMBUZI WA DATA, MATOKEO YA UTAFITI NA MJADALA..... 25

4.1 Utangulizi..... 25

4.2 *Rosa Mistika*..... 25

4.2.1 Utangulizi..... 25

4.2.2 Uhusika wa Mhusika Padri katika *Rosa Mistika*..... 26

4.2.3 Mhusika Padri kama Mtumishi wa Kanisa katika Jamii..... 27

4.2.3.1 Mhusika Padri kama Mlezi wa Kiroho 27

4.2.3.2 Mhusika Padri kama Kiongozi wa Ibada 31

4.3 *Gamba la Nyoka*..... 32

4.3.1 Utangulizi..... 32

4.3.2 Mhusika Padri katika *Gamba la Nyoka* 32

4.3.2.1 Padri kama Kiongozi wa Kanisa katika Jamii..... 33

4.3.2.2 Padri kama Mwanaume wa Kawaida katika Jamii 34

4.4 *Nagona* 40

4.4.1 Utangulizi 40
4.4.2 Padri kama Mtu Mwenye Sauti katika Jamii 41
4.4.3 Padri kama Mtu Mwenye Uwezo Kuliko Wengine 41
4.4.4 Padri kama Mwelekezaji (Mwonyesha Njia) 42
4.4.5 Padri kama Mlevi katika Jamii 43
4.4.6 Padri kama Mtu asiye na Heshima kwa Wazee 44
4.4.7 Padri kama Binadamu wa Kawaida 44
4.5 Dhamira Zinazowasilishwa na Mhusika Padri 45
4.5.1 Utangulizi 45
4.5.2 Suala la Malezi ya Kiroho 45
4.5.3 Unafiki wa Viongozi wa Kanisa Katoliki 47
4.5.4 Uonevu na Kukosekana kwa Haki 49
4.5.5 Suala la Uwezo wa Padri kuondoa Dhambi 50
4.6 Motifu Inayojitokeza kupitia Mhusika Padri 52
4.6.1 Utangulizi 52
4.6.2 Motifu ya Padri Aliyeshindwa 53
4.6.3 Mhusika wa Kimotifu (Mhusika anayewakilisha motifu) 56
4.7 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti 57
4.7.1 Mhusika Padri Anavyoelezewa katika Riwaya za Kezilahabi 57
4.7.2 Tofauti za Uwasilishaji wa Mhusika Padri katika Riwaya za Kezilahabi 61
4.7.3 Dhamira Zinazowasilishwa na Mhusika Padri 62
4.7.3.1 Dhamira ya Malezi ya Kiroho 62
4.7.3.2 Dhamira ya Unafiki wa Viongozi wa Kanisa Katoliki 63
4.7.3.3 Dhamira ya Uonevu na Kukosekana kwa Haki 67

4.7.3.4 Dhamira ya Uwezo wa Padri Kuondoa Dhambi 67

4.7.4 Motifu ya Padri Aliyeshindwa 68

4.8 Ufaafu wa Nadharia ya Uhalisia wa Kimarx Tuliyoitumia 69

4.9 Hitimisho..... 70

SURA YA TANO: **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** **72**

5.1 Utangulizi.....72

5.2 Muhtasari Kuhusu Utafiti.....72

5.3 Matokeo ya Utafiti na Ugunduzi.....73

5.4 Mchango wa Utafiti.....75

5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo.....76

MAREJELEO 77

VIAMBATANISHO..... 80

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA UTAFITI

1.1 Utangulizi

Utafiti huu unahusu usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi za *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990). Katika kazi zake mbalimbali, Kezilahabi amemtumia mara nyingi Padri kama mhusika kuliko alivyowatumia wahusika wengine. Jambo hili limevuta hamu ya utafiti kutaka kujua ni kwa nini hasa mhusika huyu amemvutia mwandishi, na hasa kutaka kumjua kwa undani mhusika mwenyewe. Katika kufanya utafiti huu lengo ni kujadili dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya hizo na kubainisha motifu inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya teule.

Sura hii imegawanywa katika sehemu saba: sehemu ya kwanza inaeleza utangulizi wa sura hii, sehemu ya pili usuli wa tatizo la utafiti, sehemu ya tatu inaeleza tatizo la utafiti, sehemu ya nne inaeleza malengo ya utafiti, sehemu ya tano inaeleza juu ya maswali ya utafiti, sehemu ya sita inaeleza umuhimu wa utafiti na sehemu ya saba inaeleza mawanda ya utafiti na sehemu ya nane ni hitimisho la sura hii.

1.2 Usuli

Wataalamu mbalimbali (Mlacha, 1985, 1986, 1987, Madumulla 1987, 2009, Wamitila 2002, Ntarangwi 2004, Njogu na Chimerah 2008, Senkoro 1982,2011) wameshughulikia wahusika katika fasihi ya Kiswahili na wote kwa namna moja au nyingine, wanakubaliana kuwa wahusika ni viumbe waliokusudiwa kuwakilisha tabia za watu katika kazi ya fasihi.

Mathalan, Mlacha (1985:30), anasema, “riwaya yoyote haikosi mhusika na mara nyingi huwapo wahusika kadhaa. Anaendelea kusema kuwa, wahusika ni watu ambao msanii mwenyewe huwabuni kutokana na maisha ya jamii yake kulingana na kile anachotaka kukifafanua”. Akifafanua umuhimu wa uhusika katika nathari, Mlacha (1986), anasema, uhusika ni moja kati ya vipengele muhimu sana vya nathari. Nafasi na dhima ya mhusika vina umuhimu mkubwa katika muundo wa matini (tafsiri ni yetu).

Kutokana na mambo haya mawili: jinsi wahusika wanavyobuniwa na dhima yao katika kazi ya kifasihi, tunaona kuwa uumbaji wa mhusika Padri katika kazi za Kezilahabi haukutokea kibahati nasibu. Mwandishi bila shaka alikuwa na lengo fulani na amemtumia mhusika wake kurejelea lengo hilo.

Msokile (1992:42), anasema, “wahusika katika kazi yoyote ya sanaa itumiayo lugha ni watu, wanyama ama vitu. Wahusika hao husawiriwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Kwa hiyo, mwandishi huwasawiri wahusika kwa wasomaji wake kwa kutumia sifa pambanuzi walizo nazo, namna gani walivyo, mambo gani hawayapendi na yapi wanayapenda, na maisha yao”. Tunaamini kuwa mwandishi kwa kumtumia mhusika Padri, zipo dhana ambazo alikusudia kuziwasilisha kwa jamii kupitia sifa pambanuzi alizo nazo mhusika huyo na namna alivyo.

Mbali na wahusika kwa ujumla, mhusika Padri ametumiwa na waandishi kadhaa. Katika kazi mbalimbali za fasihi zikiwemo za riwaya ya Kiswahili mhusika Padri

amejitokeza kwa namna tofauti. Mhusika huyu kwa mfano anatokea katika riwaya ya Juan Rulfo *Pedro Pàramo* (1955), riwaya ya *Pete* ya Komba (1986), riwaya ya *Janga Sugu la Wazawa* ya Gabriel Ruhumbika (2001) na katika riwaya tatu za Euphrase Kezilahabi yaani *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979), na *Nagona* (1990) na kwa sehemu ndogo sana katika *Mzingile* (1991).

Kwa kuwa mhusika Padri amejitokeza mara nyingi katika riwaya ya Kiswahili na zaidi katika riwaya za Kezilahabi, tumevutiwa kufanya utafiti kumhusu yeye miongoni mwa wahusika wengine kutokana na namna alivyotumika. Aidha kwa kuwa mwandishi ni miongoni mwa magwiji wa fasihi ya Kiswahili, bila shaka kwa kumtumia Padri alikuwa na lengo mahususi. Hivyo basi utafiti huu unakusudia kuchunguza usawiri wa mhusika Padri katika riwaya tatu za Kezilahabi ambazo ni *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990).

1.3 Tatizo la Utafiti

Licha ya wanafasihi mbalimbali kama vile (Senkoro 1976, Gibbe 1982, Senkoro 1982, 2011, Mulokozi 1983, Madumulla 1987, Mlacha 1986, 1987, 1988, 1991, Wamitila 1991, 1998, 2003, Bertoncini 1992, Gromov 1998, Mbatiah 1998, Diegner 2002, Mwangoka 2011) kwa kutaja tu baadhi, kushughulikia riwaya za Kezilahabi na kugusia wahusika kwa namna moja au nyingine, bado kuna pengo la kiuchambuzi kumhusu mhusika Padri. Mtazamo wa wanafasihi na watafiti walio wengi umekuwa ni kuwashugulikia wahusika kwa kuzingatia nafasi zao katika riwaya na si uhusika wao. Kwa hiyo, uchambuzi na uhakiki haujawagusa wahusika kutokana na uhusika wao kama viongozi wa siasa au dini, au serikali, n.k. Swali tunalojiuliza hapa ni je,

ni nini maana ya uhusika wa kiongozi kama huyu katika nafasi yake ya kazi katika jamii halisi (yaani jamii nje ya riwaya)? Kwa mfano, Kezilahabi anamtumia mhusika Malyangu ambaye ni katibu Mkuu wizarani (*Cha Mnyonge Utakitapika Hadharani*). Je ni nini athari na maana pana ya dhima ya makatibu wakuu wa wizara kwa namna wanavyotazamwa na mwandishi? Vivyo hivyo kwa mhusika wa kisiasa au kidini kama alivyotumika Padri.

Uchambuzi wa mhusika Padri umefanywa kwa uchache na Wamitila katika makala zake mbalimbali (1991, 1998 na 2003). Kwa mfano, katika makala yake inayojulikana kama "A Philosophical Labyrinth: Tracing two Critical Motifs in Kezilahabi's Prose Works" Wamitila (1998) anaizungumzia riwaya ya *Rosa Mistika* kwa kusema kuwa, mwandishi anaonesha mapungufu ya Ukristo wakati Padri wa Kikatoliki anapokwenda kumshauri Rosa lakini hachukui hatua yoyote ya kuzungumzia matatizo yake (Rosa) ya hapa hapa duniani na badala yake anaegemea zaidi kwenye maono ya kesho nzuri (tafsiri ni yetu). Akimwangalia Padri katika *Gamba la Nyoka* Wamitila (keshatajwa uk 84) anaendelea kudai kwamba, matumizi ya Padri yanaendeleza unafiki mkubwa na ulioenea katika Ukristo. Kupitia kwa Padri Madevu na mmoja wa wafuasi wake waaminifu, Mama Tinda, dhamira ya unafiki inajieleza wazi kwa mujibu wa Wamitila. Ingawa uchambuzi huu wa Wamitila kuhusu uhusika wa Padri katika kazi za Kezilahabi unaongezea hamu na maswali ya kiutafiti kazi yake haiingii ndani na kufanya uchambuzi wa kina.

Kwa mfano, Padri yupo huru kiasi gani ili aishi kama mtu huru katika jamii? Je, anashikiliwa na miiko ya kazi yake, au miiko ya mazingira anamoishi? Je, uhusika

wake unamwakisi yeye kama kiumbe mwenye imani, au utashi binafsi? Je, ni nini kinachomjenga kama Padri? Bila kujua ni kwa kiasi gani Padri ni mhusika huru au tegemezi wa hali au mazingira fulani, wachambauzi hawawezi kumfahamu kwa undani mhusika wanayetaka kumchambua. Je, Padri anapofanya maamuzi yake, anayafanya kama mwanamume mwingine yeyote au kama Padri? Je, kuna mahali tunapoweza kumtofautisha mhusika anapofanya maamuzi yake kama kiongozi wa dini na pengine anapofanya maamuzi kama mwanamume katika jamii?

Kukosekana kwa utafiti wa kinadharia juu ya mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi kunaleta ugumu katika kuamua iwapo tabia, mwenendo pamoja na matendo ya mhusika huyu yanaamuliwa na asasi ya dini ya Kikristo au utashi binafsi. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu ukiongozwa na nadharia ya Uhalisia wa Kimarx, unachunguza usawiri wa mhusika Padri katika riwaya tatu za Kezilahabi *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990).

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu unaongozwa na lengo la jumla na malengo mahususi

1.4.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi, *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990)

1.4.2 Malengo Mahususi

(i) Kumchambua Mhusika Padri na uhusika wake katika riwaya teule

(ii) Kujadili dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya teule

(iii) Kubainisha motifu inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya teule

1.5 Maswali ya Utafiti

(i) Je, tunaweza kumchambuaje mhusika Padri na uhusika wake katika riwaya teule?

(ii) Je, ni dhamira zipi zinawasilishwa na mhusika Padri katika riwaya teule?

(iii) Je, kuna motifu yoyote inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya teule?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu ufuatao kitaaluma:-

Kwanza,utafiti huu utawasaidia wasomaji na watafiti wa fasihi hususan katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili kuzielewa vizuri riwaya teule zitakazofanyiwa uchunguzi.

Pili, utafiti huu unakusudia kujadili dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya zitakazoshughulikiwa pamoja na kubainisha motifu inayojitokeza katika riwaya teule kupitia mhusika Padri, na mahitimisho yatakayotolewa yatasaidia kuonesha iwapo maamuzi na matendo ya mhusika huyu yanaongozwa na asasi ya dini ya Kikristo au utashi binafsi.

Tatu, utafiti huu utatumika kama rejeleo muhimu kwa watafiti wengine watakaoamua kufanya utafiti juu ya wahusika katika riwaya za Kezilahabi na wale watakaotafiti kuhusu mhusika Padri katika riwaya nyingine za Kiswahili.

Nne, utafiti huu utatusaidia kubaini mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi ni aina gani ya mhusika

1.7 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na kwa sehemu ndogo kwa mahojiano na mwandishi kwa njia ya simu. Mtafiti alisoma kazi mbalimbali za Euphrase Kezilahabi pamoja na kazi za waandishi walioandika kuhusu wahusika na ulijikita katika riwaya tatu za Kiswahili zilizoandikwa na Kezilahabi ambazo ni *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990). Ulichunguza namna mhusika Padri anavyosawiriwa katika riwaya hizo, dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya hizo pamoja na motifu inayojitokeza kutokana na mhusika Padri katika riwaya zote tatu. Sababu ya kuchagua riwaya hizi ni kutokana na kujitokeza kwa mhusika Padri katika riwaya zote tatu zilizotajwa. Kazi nyingine za Kezilahabi hazikushughulikiwa. Utafiti huu haukushughulikia kazi nyingine za fasihi kama tamthiliya na ushairi au riwaya za Kiswahili za waandishi wengine.

1.8 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili vipengele vya utangulizi kwa ujumla, usuli, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mawanda ya utafiti. Tumeona kwa ufupi umuhimu wa kufanya utafiti huu hususan haja ya

kumwelewa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi ili tuweze kujua iwapo maamuzi yake yanaongozwa na asasi ya dini anayoiwakilisha au utashi binafsi.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sehemu hii inawasilisha mawazo makuu yatokanayo na mapitio ya maandiko mbalimbali. Mawazo hayo yanahusiana na mada yetu ya utafiti. Tafiti na chambuzi zimepatikana katika vitabu, majarida mbalimbali, tasinifu na kupitia mtandao wa intaneti. Katika sura hii tutaweza kuona jinsi ambavyo watafiti mbalimbali wamechambua kazi za Kezilahabi pamoja na mianya iliyoachwa na ambayo ni lengo la utafiti huu kuiziba. Pia nadharia iliyotumika kama mwega wa utafiti wetu imeelezwa katika sehemu hii.

2.2 Tafiti Tangulizi na Mapitio ya Maandiko

2.2.1 Mapitio ya riwaya za Kezilahabi kwa Ujumla

Riwaya za mwanzo za Kezilahabi zimechambuliwa kwa mapana kwa kutumia mbinu za kimuundo (Mlacha 1986, 1987 na 1991). Riwaya mbili za *Nagona* na *Mzingile* zimechambuliwa kwa lengo la kuona dhamira kuu (Chenou 1997). Suala la tanzu katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* limeshughulikiwa na (Gromov 1998) na suala la motifu za kifalsafa limeshughulikiwa na (Wamitila 1991, 1998 na 2003). Naye Diegner (2002) ameshughulikia suala la istiara katika riwaya za mwanzo za Kezilahabi. Pia ziko tafiti za karibuni kuhusu wahusika katika riwaya ya Kiswahili (Kanwa 2011, Chaligha 2011, Mukama 2011, Lyatuu 2011, na Nkinde 2011. Nkinde (keshatajwa) alifanya utafiti wake juu ya motifu za safari na msako katika makuzi ya wahusika wa riwaya za Kezilahabi. Ingawa Nkinde anamtaja mhusika Padri katika

utafiti wake hakujikita sana katika kumchambua mhusika huyu kwani halikuwa lengo lake la utafiti.

Gibbe (1982) katika makala yake "Baadhi ya Taswira katika *Gamba la Nyoka*" ameshughulikia taswira mbalimbali zinazojitokeza katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*. Ingawa mwandishi wa makala haya amemgusia mhusika Padri Madevu kutokana na taswira zinazoibuliwa na kauli zake, bado hakuna uangavu wa kutosha kumhusu mhusika huyu kutokana na sababu kubwa kwamba halikuwa lengo la mwandishi kuzungumzia usawiri wa mhusika Padri kwa mapana yake.

Mlacha (1987) katika makala yake ya "Aggression as a Mental and Social Disorder: A Study of Swahili Novels," ameshughulikia riwaya mbalimbali za Kiswahili. Miongoni mwa riwaya za Kezilahabi zilizoshughulikiwa katika makala hayo ni *Rosa Mistika, Kichwa Maji*, *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Gamba la Nyoka*. Katika makala hayo mwandishi anawaangalia wahusika mbalimbali kwa kigezo cha kimuundo. Hata hivyo mhusika Padri hakugusiwa kabisa ingawa anatokea katika riwaya za *Rosa Mistika* na *Gamba la Nyoka* alizozishughulikia.

Makala za Wamitila (1991, 1998, 2003) zimemgusia mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Wamitila (keshatajwa) katika makala zake hizo anamwona Padri kama mwakilishi wa asasi ya dini ya Ukristo na hivyo kumchukulia Padri katika riwaya za Kezilahabi kuwa anawakilisha mapungufu na unafiki wa Ukristo. Hata hivyo pamoja na kumzungumzia mhusika Padri, mtazamo wake kwa maoni yetu ni wa jumla mno na haumwezeshi msomaji wa kazi za Kezilahabi zinazomzungumzia mhusika Padri

kumwelewa mhusika huyo ipasavyo na iwapo maamuzi yake yanaongozwa na utashi binafsi au dini ya Ukristo.

Ni kutokana na mantiki hiyo, ndipo tumeona iko haja ya kufanya utafiti wa usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990)

2.2.2 Mapitio ya Maandiko kuhusu Aina za Wahusika

Mlacha (1985:42-44), amegawa wahusika katika makundi matatu ambayo ni wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Mlacha anaendelea kusema kuwa wahusika wakuu ndio nguzo na hasa ndio wanaoshikilia hadithi nzima. Matendo yote yamejengwa kuwahusu au kutokana na wao. Wahusika wengine wote wanahusishwa na wahusika hawa wakuu.

Mlacha (amekwishatajwa: 43) anazidi kusema kuwa, wakati tunapozungumzia aina za wahusika, makundi haya matatu lazima tuyazingatie. Ni muhimu kwa vile ndiyo hasa yanayoijenga riwaya nzima. Sababu ya pili ni kuwa, aina yoyote ya mhusika itakuwa imetokana na jinsi msomaji anavyomwona mhusika huyo katika uhusiano wake na makundi hayo na pia kwa kulinganishwa ili aweze kupata kundi la aina yake. Mlacha anaendelea mbele zaidi ambapo anayagawa makundi hayo matatu ya wahusika katika aina nyingine tatu za wahusika ambao ni: wahusika bapa, anaowagawa katika makundi mawili ya sugu na kielelezo, wahusika duara na wahusika shinda. Tunakubaliana na Mlacha kuwa wahusika wakuu ni muhimu zaidi katika riwaya. Hata hivyo tunaona kuwa upo umuhimu wa kuwachunguza wahusika

wengine kwa undani. Kwa upande mwingine pia haieleweki ni kigezo gani kinachotumika kupata wahusika hawa. Je, ni maudhui? Kujitokeza kwao mara nyingi au ni nini haswa?

Mohamed (1995), anasema, “wahusika ni viumbe vya mawazoni vinavyoumbwa na mwandishi na kuibuka katika kazi yake ya fasihi”. Mohamed (amekwishatajwa: 73-74), anataja aina tatu za wahusika ambao ni**:** mhusika mviringo-mhusika anayemkaribia mno mwanadamu kwa ulinganifu wa wasifu na tabia na kwa hivyo anaaminika na kukubalika katika kipimo cha ukweli wa uhalisi wa maisha. Mhusika bapa na mhusika kinyago-huyu ni mhusika ambaye huchorwa kutokana na haja ya mwandishi kukejeli tabia fulani ya kuchukiza kwa njia ya tashtiti au kichekesho. Kwa jina jingine twaweza kumwita kerekecha. Upungufu uliojitokeza kwa Mlacha wa kutokubainisha wazi vigezo vinavyotumika katika kuwapata wahusika hao unajitokeza hapa pia.

Madumulla (2009:141-142), amewachambua wataalamu mbalimbali wa fasihi waliojadili kuhusu wahusika kama vile Senkoro, Njogu na Chimerah na hatimaye akahitimisha kwa kusema kuwa, “si rahisi sana kubainisha njia muafaka ya kuainisha wahusika”. Madumulla (amekwishatajwa), anaendelea kusema kuwa, hata hivyo, “kuna makundi makuu mawili tu ya wahusika: Wahusika wakuu na Wahusika wadogo au wasaidizi. Kila kundi katika hayo mawili linaweza kuwa na sifa za: Uduara- kwa maana kwamba ni wahusika halisi wenye sifa kamili za mtu, wenye mchangamano wa uzuri na ubaya, na wanaokua kiakili, kimwili na kisaikolojia na wenye kubadilika badilika. Ubapa- wahusika wasio na sifa za kukua

na kubadilika; waliotuama kiakili na kisaikolojia. Uvuli au ufoili- wasiojitokeza sana, lakini wako karibu sana, na wanashirikiana na mhusika mkuu. Kwa mfano Najum ni mhusika foili wa Bwana Msa; Ukikaragosi- wenye kushabikia na kutumikia wengine; Ubabe na kadhalika".

Kimsingi tunakubaliana na Madumulla kuwa upo ugumu katika kuainisha wahusika. Pia kuweka wahusika katika makundi mawili tu kunaleta urahisi katika uchambuaji na uainishaji wa wahusika kwa namna moja au nyingine. Hata hivyo bado tunabaki na swali juu ya kigezo alichotumia kupata makundi hayo mawili ya wahusika.

Jericho (2012: kutoka mtandaoni) anasema, katika fasihi, waandishi hutumia aina nyingi tofauti za wahusika kusimulia hadithi zao. Wahusika tofauti tofauti hutimiza malengo mbalimbali katika mchakato wa usimuliaji, na ukiwachambua unaweza kupata aina zifuatazo za wahusika (tafsiri ni yetu):

(a) **Wahusika wakuu** ambao ni muhimu katika ujenzi na suluhisho la mgogoro. Kwa maneno mengine, ploti na suluhisho na mgogoro huwazungukia wahusika hawa (tafsiri ni yetu)

(b) **Wahusika wadogo** huwakamilisha wahusika wakuu na kusaidia kusukuma matukio ya ploti mbele (tafsiri ni yetu)

(c) **Mhusika endelevu (*dynamic*).** Ni mhusika ambaye hubadilika kulingana na wakati, mara nyingi kutokana na kusuluhisha mgogoro mkubwa au kukutana na tatizo kubwa. Wahusika endelevu walio wengi huwa wahusika wakuu badala ya wahusika wadogo (*peripheral characters*) kwa

sababu kusuluhisha mgogoro ndiyo kazi kuu ya mhusika mkuu (tafsiri ni yetu)

(d) **Mhusika tuli (*static*).** Ni yule asiyebadilika kulingana na wakati, utu wake haubadiliki (tafsiri ni yetu)

(e) **Mhusika duara (*round*).** Ni mhusika yeyote ambaye ana haiba changamani. Mara kwa mara husawiriwa kama anayetatizika na asiyeeleweka (contradictory). (tafsiri ni yetu)

(f) **Mhusika Bapa.** Ni kinyume cha mhusika duara. Utu huu wa kifasihi unatambuliwa kwa aina moja tu ya sifa. (tafsiri ni yetu)

(g) **Wahusika Stoku/Akiba.** Ni aina ya wahusika ambao wamezoeleka kutokana na kutumiwa mara kwa mara katika baadhi ya hadithi. (tafsiri ni yetu)

(h) **Protagonisti.** Ni mtu muhimu katika hadithi na mara kwa mara anajulikana kama mhusika mkuu katika simulizi**.** Hukutana na mgogoro ambao sharti utatuliwe. (tafsiri ni yetu)

(i) **Antagonisti.** Ni mhusika/wahusika au hali ambayo hutoa upinzani ambao ni lazima protagonisti akutane nao. Kwa maneno mengine, antagonisti ni kikwazo ambacho protagonisti analazimika kukivuka (tafsiri ni yetu).

(j) **Pinga-Shujaa** (*Anti-Hero*). Ni mhusika mkuu, kwa kawaida protagonisti, ambaye hana ufahamu uliozoeleka, na ambaye anatafuta/anapenda mambo yasiyokubalika na wengi. Hana adabu (vulgar), ana hila na ni mbinafsi. (tafsiri ni yetu)

(k) **Mhusika Foili.** Ni mhusika yeyote (kwa kawaida huwa antagonisti au mhusika msaidizi muhimu) mwenye sifa zinazokinzana na za mhusika

mwingine (kwa kawaida huwa protagonisti). Kwa kutoa ukinzani huu, tunapata kumfahamu zaidi huyo mhusika wa pili (protagonisti) (tafsiri ni yetu).

(l) **Mhusika wa Kiishara (*Symbolic Character*)**. Ni mhusika yeyote mkuu au msaidizi/mdogo, ambaye kuwapo kwake huwakilisha baadhi ya mawazo makuu au dhana fulani katika jamii (tafsiri ni yetu).

Tunaweza kuona kuwa suala la uainishaji wa wahusika linategemea sana mtazamo wa mwandishi. Ni vigumu kukubaliana kuhusu kigezo haswa ambacho chafaa kutumika katika uainishaji wa wahusika kwani kila mmoja anao mtazamo wake ambao ni tofauti na wa mwingine. Hata hivyo tunaweza kuona kuwa kwa namna moja au nyingine kuna hali ya kufanana au kukubaliana kwa namna fulani baina ya wataalamu mbalimbali haswa kuhusu suala la wahusika wakuu na wahusika wadogo. Wengi wanazungumzia kuhusu wahusika wakuu na wahusika wadogo au wasaidizi. Suala muhimu hapa ni je, wametumia kigezo cha matumizi au kazi kuwapata wahusika hao?

Swali letu hapa ni je, mhusika Padri anayejitokeza katika riwaya za Kezilahabi anaingia katika kundi gani? Je, ni mhusika mdogo, au mhusika msaidizi? Jibu lolote haliwezi kujitosheleza kutokana na sababu kubwa moja: hakuna utafiti wa kinadharia uliofanywa hata sasa kumhusu mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Kwa upande mwingine bado tunabaki na maswali kama vile: Je, mhusika Padri anabeba wazo lilelile kila anapojitokeza au anabeba wazo/dhamira tofauti tofauti katika kila riwaya? Je, katika *Nagona* ambapo tuna mhusika jumui (wahusika wengi katika mmoja na Padri akiwemo) mhusika Padri anabeba wazo

jipya au ni wazo lile lile? Je, mhusika Padri ni mhusika aliyezoeleka au ni aina mpya ya mhusika katika riwaya ya Kiswahili? Maswali haya na mengine yanatokeza haja ya kufanya utafiti wa kinadharia kuchunguza usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi kama inavyofanyika katika utafiti wetu.

2.3 Kiunzi cha Nadharia

2.3.1 Utangulizi

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uhalisia wa Kimarx ambayo waasisi wake ni Karl Marx na Fredrich Engels.

2.3.2 Maana ya Uhalisia wa Kimarx

Wamitila (2002) anasema kuwa Uhalisia ni dhana inayotumiwa katika fasihi kuelezea hali ilivyo katika jamii kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Uhalisia ni dhana muhimu katika uhakiki wa fasihi na ina historia ndefu. Uhalisia ulizuka kama vuguvugu la kuupinga mtazamo wa Kiromansia. Ni mkondo unaosisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Mmoja wa wafuasi wa nadharia hii ni Georg Lukacs ambaye anaamini katika usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake na kuchunguza undani wa picha inayoonekana ya uhalisi na kugundua sheria za mabadiliko ya kihistoria zinazosababisha hali fulani.

Ntarangwi (2004: 48-49) anatueleza kwamba, “nadharia hii katika upana wake, humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa hususan kwa sababu za kupinga mkondo wa

ulimbwende. Mhalisia huamini katika matokeo ya mambo na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba. Vilevile, wahalisia huiamini demokrasia kama hali ya maisha, na malighafi anayochagua kueleza maisha ni yale ya kawaida, ya kadiri na ya kila siku. Hivyo basi, uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahsusi, na matokeo yanayoweza kuthibitika. Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli, na halisi. Hivyo basi hata picha za ulimwengu atakazoumba msanii, zapaswa kudhihirisha hali hiyo. Kama tulivyotaja hapo juu, uhalisia ulizuka ili kupinga uromansia ambao ulizingatia mambo ya kihisia na yasiyo halisi maishani. Wahalisia wanaona kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwa sahihi, iliyo wazi na inayozingatia masuala halisi moja kwa moja bila kupiga chuku. Masuala ya kati maishani huhusu maadili na hivyo basi msanii hana budi kuyazingatia kwa kiwango fulani cha uteuzi. Wahalisia wanashikilia kwamba msanii anapaswa kuteua lakini akiwa na nia ya kuendeleza maswala yake kama yanavyowahusu watu katika hali halisi za maisha. Mwelekeo huu wa uhalisi katika utunzi unamfanya mhalisia kumwona mhusika kama kiungo muhimu sana katika kazi ya fasihi (hususa riwaya). Hivyo basi, anazingatia saikolojia ya wahusika katika hadithi.

Mhakiki anayezingatia nadharia hii ya uhalisia, hupembua namna mtunzi alivyodhihirisha uhalisi wa mambo kupitia maudhui aliyoyazingatia na wahusika aliowasawiri. Hivyo basi, mhakiki hutazama jinsi ukweli ulivyodhihirishwa katika juhudi za mtunzi za kuchora hali halisi ya mambo katika wakati maalum. Kwa muhtasari basi msanii anatarajiwa kusawiri wahusika, matukio na mandhari

yanayokubalika na kuaminika katika jamii ya wakati wake. Ufahamu wa mazingira na maisha anayoyalenga mtunzi ni nguzo muhimu kwa mhakiki wa kihalisia.

Katika utafiti huu tunakusudia kueleza namna mhusika Padri anayosawiriwa katika riwaya za Kezilahabi *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990) kwa kuhusianisha na hali halisi ya sasa kulingana na usawiri huo katika riwaya teule. Uhalisia utajidhihirisha kupitia maneno na matendo ya mhusika Padri katika riwaya teule. Tumeichagua nadharia hii kwa sababu tumeona ndiyo inayofaa zaidi katika kuelezea usawiri wa wahusika kwani inataka kuona ni kwa jinsi gani mwandishi amedhihirisha uhalisi kwa kupitia dhamira zinazoibuliwa na wahusika aliowatumia. Katika utafiti wetu huu, tunamwangalia mhusika mmoja ambaye ni Padri.

2.4 Hitimisho

Sura hii imepitia maandiko mbalimbali kuhusu riwaya za Kezilahabi na tafiti zilizofanywa kuhusu riwaya hizo kwa ujumla. Tumejadili kuhusu maandiko yanayoelezea kuhusu wahusika na kuona ugumu uliopo katika uainishaji wa wahusika. Pia tumeeleza kuhusu nadharia ya Uhalisia wa Kimarx iliyotumika kama mwega wa utafiti wetu na sababu zilizotufanya tuamue kuitumia nadharia hiyo.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Kiini cha sura hii ni mbinu za utafiti, ikijumuisha mbinu za ukusanyaji data, uchakataji data, sampuli na usampulishaji, eneo la utafiti pamoja na vifaa vilivyotumika katika utafiti.

3.2 Mbinu za Ukusanyaji Data

Utafiti huu ulihusisha mbinu ya Uchambuzi Matini na mahojiano katika kufikia malengo ya utafiti pamoja na mbinu nyingine mbalimbali kama vile mbinu ya kujisomea na tajiriba/uzoevu binafsi.

3.2.1 Uchambuzi Matini

Kothari (2004:110) anasema Uchambuzi Matini ni mbinu ya kukusanya data na taarifa mbalimbali kutoka katika vitabu, majarida, na magazeti pamoja na matini zingine ambazo zinaweza kuwa simulizi au zilizondikwa. Mbinu hii ilitumiwa kukusanya data za msingi kutoka katika riwaya za *Rosa Mistika* (1971). *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990). Data za msingi zilizokusanywa kwa njia ya uchambuzi matini na kujisomea binafsi ni pamoja na:-

(i) Maelezo kuhusu kile anachokisema mhusika Padri na kwa vile anavyokisema katika riwaya tatu teule.

(ii) Maelezo juu ya kile mhusika Padri anachokifanya katika riwaya tatu teule.

(iii) Taarifa za yale ambayo wahusika wengine wanasema kumhusu mhusika Padri katika riwaya tatu teule.

(iv) Taarifa za mazingira yanayomzunguka mhusika Padri katika riwaya tatu teule.

(v) Taarifa zinazohusu mwitikio wa mhusika Padri kwa wahusika wengine katika riwaya tatu teule.

Data hizi zilirekodiwa katika shajara na kufanyiwa uchambuzi kulingana na malengo ya utafiti.

Data fuatizi zilikusanywa kutoka katika maandiko mbalimbali ambayo yanapatikana katika kitengo cha makusanyo cha '*East Africana'* na makusanyo ya Sayansi za Jamii katika maktaba kuu ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Maktaba nyingine ambazo zilitumika ni pamoja na ile ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam pamoja na kwenye mtandao. Aidha, data fuatizi zilipatikana pia katika gazeti la *Risasi* na katika Biblia Takatifu.

Data fuatizi zilizopatikana kwa njia ya uchambuzi matini na usomaji binafsi ni kama vile:-

(i) Maelezo yanayohusu nadharia ya Uhalisia wa Kimarx iliyotumika katika utafiti wetu.

(ii) Taarifa zinazohusu aina za wahusika na kadhalika.

Data hizi zilirekodiwa katika shajara na baadaye kutumiwa katika utafiti wetu kwa lengo hoja na mjadala.

3.2.2 Mahojiano

Kothari (2004) anasema, mbinu ya kukusanya data kwa njia ya mahojiano inahusisha uwasilishaji wa maswali kwa njia ya mdomo na majibu kutolewa kwa njia ya mdomo. Mbinu hii inaweza kutumika kupitia mahojiano binafsi na kama inawezekana mahojiano ya simu.

Katika utafiti huu tulikusudia kufanya mahojiano ya uso kwa uso na mwandishi Euphrase Kezilahabi. Kwa kuwa haikuwezekana kumpata kwa mahojiano ya uso kwa uso tulitumia mbinu ya mahojiano kwa njia ya simu ambayo yalifanyika tarehe 24, Mei, 2013 saa saba kamili mchana. Mbinu ya mahojiano ilitusaidia katika kupata taarifa muhimu zinazohusiana na utafiti wetu. Data zilizopatikana kwa njia ya mahojiano ni pamoja na:-

(i) Taarifa juu ya jambo lililomsukuma mwandishi kuandika riwaya ya *Rosa Mistika.*

(ii) Taarifa za maisha ya awali ya mwandishi akiwa seminarini.

Taarifa zilizopatikana zilirekodiwa kwa njia ya kinasa sauti na kutumiwa wakati wa kuandika ripoti ya utafiti hususan kwa lengo la kukazia hoja.

3.3 Sampuli na Usampulishaji

Kothari (2004:152) anasema, usampulishaji ni mchakato wa kupata taarifa kuhusu Wango kubwa kwa kuitathimini sehemu tu ya wango hilo (tafsiri yetu). Wango lengwa katika utafiti wetu ni riwaya tatu za Kezilahabi ambamo mhusika Padri anajitokeza. Riwaya hizi zimeteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa, yaani, mtafiti aliteua watafitiwa au vitafitiwa ambavyo aliamini kuwa watampatia au

vitampatia data na taarifa sahihi zilizosaidia kujibu maswali ya utafiti wake. **Sampuli** ni sehemu ya jamii au vitu fulani. Utafiti huu ulitumia **Sampuli Nasibu**. Hii ni aina ya sampuli ambayo hutoa nafasi sawa kwa memba wote kupata nafasi ya kushiriki katika sampuli ya utafiti. Riwaya zote tatu zilisomwa kwa makini na kila mahali ilipoonekana mhusika Padri anajitokeza moja kwa moja au kwa kuzungumziwa na wahusika wengine data ilinukuliwa katika shajara.

3.4 Uchambuzi, Uchakataji na Uwasilishaji wa Data

Baada ya zoezi la ukusanyaji wa data kukamilika, data zilizokusanywa zilichambuliwa, kujadiliwa na kuwasilishwa.

(Kothari 2004:122) anasema, uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika.

Katika uchambuzi wa data, utafiti huu uliongozwa na mbinu ya uchambuzi wa kifasihi. Uchambuzi huu ulihusisha hatua nne. Hatua ya kwanza ni kukusanya data kwa njia ya uchambuzi wa riwaya zilizoteuliwa na kwa njia ya mahojiano na mwandishi wa riwaya hizo. Hatua ya pili ni kuchambua uhusika wa mhusika Padri katika riwaya teule. Hatua ya tatu ni kujadili dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya teule. Hatua ya nne ni kubainisha motifu inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya teule. Uchambuzi wa data ulifanywa kulingana na maswali ya utafiti.

Data zilizokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali kwa njia ya uchambuzi wa matini na kwa njia ya mahojiano na mwandishi, zilichambuliwa na kufupishwa kwa kutumia mkabala usio wa kiidadi au mkabala wa kimaelezo. Baada ya uchambuzi, data ziliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Kwa kutumia mkabala wa kimaelezo, maeneo mbalimbali ya usawiri wa mhusika Padri katika riwaya teule yameelezwa, dhamira mbalimbali zinazowasilishwa na mhusika Padri zimejadiliwa na motifu inayojitokeza kupitia mhusika Padri imebainishwa. Mkabala huu umetumika kwa sababu uchanganuzi wa data ulifanywa kwa njia ya maelezo na ndio muafaka kwa utafiti wa kutoa maelezo.

3.5 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vilivyohitajika katika kufanikisha utafiti wetu ni pamoja na kompyuta, karatasi, kalamu, shajara, pamoja na tepurekoda. Kompyuta ilitumika kuchapa na kuhifadhi data. Pia taarifa nyingine zilipatikana kwa njia ya mtandao ambao unahusisha Kompyuta. Kalamu ilitumika kuandikia data zote zilizopatikana maktabani zisisahaulike. Shajara ilitumika kama kifaa ambamo data zote zilizopatikana katika maandiko mbalimbali zilinukuliwa . Karatasi nazo zilitumika kuandikia data zilizopatikana katika utafiti. Tepurekoda ilitumika kurekodi mahojiano yaliyofanywa kati ya mtafiti na mwandishi wa riwaya teule.

3.6 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na kwa sehemu ulihusisha mbinu ya mahojiano kwa njia ya simu. Mahojiano na mwandishi wa riwaya teule yalifanyika siku ya Ijumaa, tarehe 24, Mei 20113 saa saba mchana. Maktaba zilizotumika ni pamoja na

maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Maktaba na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). Pia mtafiti alitumia njia ya kielektroniki (wavuti na tovuti) kwa lengo la kukamilisha utafiti wake.

3.7 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili mbinu mbalimbali zilizotumika katika utafiti wetu. Tumeona mbinu za ukusanyaji data, mbinu za uchakataji wa data, sampuli na usampulishaji, eneo la utafiti pamoja na vifaa vilivyotumika katika utafiti wetu.

SURA YA NNE

UCHAMBUZI WA DATA, MATOKEO YA UTAFITI NA MJADALA

4.1 Utangulizi

Mada kuu ya sura hii ni uchambuzi wa data, matokeo ya utafiti na mjadala. Data za msingi zilitokana na riwaya teule za Kezilahabi, yaani, *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990) na zilitumika kuchambua uhusika wa mhusika Padri, kujadili dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri pamoja na kubainisha motifu inayojitokeza kupitia mhusika Padri. Uchambuzi huu wa data unakamilika kwa kusaidiana na data za upili kutoka katika maandiko na machapisho mbalimbali. Mbinu ya uchakataji wa data kwa njia ya maelezo, yaani uchakataji usio wa kiidadi ndiyo inayotumika katika kufikia malengo ya sura hii. Mjadala wa matokeo ya utafiti ulifanyika kwa kuzingatia maswali ya utafiti, mahojiano na mwandishi, taarifa zilizopatikana kutokana na utafiti huu, data za upili zilizopatikana katika magazeti na maandiko mengine, uzoefu pamoja na hali halisi katika jamii.

4.2 *Rosa Mistika*

4.2.1 Utangulizi

Riwaya ya *Rosa Mistika* ni miongoni mwa riwaya zinazotumika kama data msingi katika utafiti huu. Riwaya hii iliandikwa na Euphrase Kezilahabi mwaka 1971. Riwaya hii imejikita kwa kiasi kikubwa katika kueleza maisha ya mhusika wake mkuu Rosa.

Ni riwaya mojawapo ya kipindi ambacho waandishi walianza kuzama katika kuhakiki uhalisia wa mambo katika jamii. Katika riwaya hii, mwandishi kwa

kumtumia mhusika wake mkuu Rosa, anaonesha jinsi ambavyo malezi ya ukali na kunyimwa uhuru yanavyoweza kuchangia kuangamiza badala ya kujenga. Dhamira kuu ya riwaya hii ni malezi. Mhusika Padri anahusiana na mhusika mkuu Rosa kwani Padri anashiriki katika kumlea Rosa kiroho. Lengo letu ni kumchunguza mhusika Padri, kati ya wengine wengi wanaojitokeza katika riwaya hii.

4.2.2 Uhusika wa Mhusika Padri katika *Rosa Mistika*

Jericho (2012: kutoka mtandaoni), anataja njia kumi ambazo kwazo mhusika anaweza kufichuliwa au kutambuliwa. Njia hizo ni:

(i) Kwa maelezo ya kisaikolojia

(ii) Kwa maelezo ya kimaumbile

(iii) Kwa kudokeza vile mhusika anavyofikiri

(iv) Kwa kile anachosema

(v) Kwa vile anavyokisema

(vi) Kwa kile anachofanya

(vii) Kwa yale ambayo wengine wanasema kumhusu

(viii) Kwa mazingira yake

(ix) Kwa mwitikio wake kwa wengine

(x) Kwa mwitikio wake kwake mwenyewe (tafsiri ni yetu)

Utafiti huu umetumia baadhi ya njia hizo hususan njia za: kwa kile anachokisema, kwa vile anavyokisema, kwa kile anachofanya, kwa yale ambayo wengine wanasema kumhusu, kwa mazingira yake, na kwa mwitikio wake kwa wengine. Njia hizo ndizo zilizotuwezesha kuamua nafasi mbalimbali za mhusika Padri katika riwaya ya *Rosa Mistika* na riwaya nyingine teule za Kezilahabi.

4.2.3 Mhusika Padri kama Mtumishi wa Kanisa katika Jamii

Nafasi ya mhusika Padri kama mtumishi wa Kanisa katika jamii inajidhihirisha kupitia wajibu wake wa Kikanisa katika jamii. Hapa tunatumia kigezo cha kile anachofanya mhusika Padri kama alivyoainisha (Jericho 2012). Katika riwaya ya *Rosa Mistika,* tunamwona mhusika Padri akifanya uhusika wake kama mtumishi wa Kanisa kutokana na yale anayoyafanya. Katika riwaya hii, tunamwona mhusika Padri akiwa na majukumu makuu mawili. Majukumu hayo ni:

(i) Jukumu la malezi ya kiroho na;

(ii) Jukumu la ibada (shughuli ya mazishi).

Hebu sasa tuyachambue majukumu haya ili kuona jinsi ambavyo uhusika wa mhusika Padri unajitokeza

4.2.3.1 Mhusika Padri kama Mlezi wa Kiroho

Katika jukumu la malezi ya kiroho tunamwona mhusika Padri akitumwa kwenda kwa mhusika Rosa kwa lengo la kumwonyesha njia ya wokovu, mwandishi anasema maneno haya:

> "Rosa sasa alikuwa amekwishajulikana Morogoro nzima,
> Hata mjini. Mwishowe sifa yake iliwafikia mapadri wa pale. Padri mmoja alitumwa kwenda kumwonyesha tena mwanga wa wokovu. Padri alipofika pale shuleni aliuliza chumba cha Rosa……Aliongozwa mpaka chumba cha Rosa.
> Rosa alikuwa akisoma daftari lake aliposikia hodi mlangoni.
> Rosa alifungua mlango na Padri aliingia, Biblia yake mkononi. (1971: 47)

Katika dondoo hili tunamwona mhusika Padri kama kiongozi wa kiroho mwenye jukumu la kutoa malezi ya kiroho. Hii ndiyo sababu Padri anatumwa kwa Rosa kwa lengo la kumrejesha tena (Rosa) katika njia ya wokovu. Hata hivyo, mwandishi anaonesha kuwa Padri ameshindwa kulitimiza jukumu lake hili kutokana na kushindwa kuhusisha malezi ya kiroho na mazingira/maisha halisi. Hivi ndivyo anavyosema mwandishi katika ukurasa 48-49. Mwandishi anasema,

> Kama padri angalizungumza juu ya mambo haya labda
> Angaliweza kumsaidia. Lakini yeye alianza kuzungumzia juu ya wokovu. Kwa hiyo padri alipoanza kuzungumza, Rosa aliona anapoteza muda wake.
> "Rosa, maneno uliyoandika uliyatoa wapi?" Padri aliuliza kwa unyenyekevu. "Nimeyatoa kwa wenzangu."
> "Ninakuomba uyachome yote." Padri alinyamaza kwa muda.
> Alizungumza tena. "Rosa, nimekuja kukusaidia; nimekuja kukuonyesha tena mwanga wa wokovu."
> "Umekuja kunisaidia! Mimi maskini?"
> Ndiyo, wewe maskini wa roho."
> "Umejuaje, wewe Mungu?"
> "Mwovu huonekana kwa matendo."
> "Umeyafahamuje matendo yangu?"
> "Dalili ya moto ni moshi. Hujapata mimba wewe hata mara moja?" "Ya nani?"
> "Si lazima nifahamu ya nani."
> "Utaona kama nitapata mimba tena."
> "Mimi mtumishi wa Mungu. Nimekuletea habari njema, Rosa."
> Padri alifungua Biblia yake, pale alipokuwa ameweka picha ya mtu msalabani. Rosa alijaribu kusikiliza padri alipoanza kusoma.
> ….Padri alifunga Biblia yake. Alianza kumhubiria Rosa:
> "Usikate tamaa. Rosa usikate tamaa…..Wokovu bado uko machoni mwako."
> Rosa alianza kutapika maneno, na matapishi hayamezwi tena. "Wokovu maana yake nini? Wokovu! Wokovu gani! Kama kuna moto basi nitakwenda!"
> "Rosa usihamaki."
> "Hapana; hufahamu taabu zilizonipata."
> "Padri maisha yangu yamekwishaharibika, na sijali! Kwa nini wewe ujali roho yangu kuliko mimi mwenyewe?"
> Padri alimwangalia, alishangaa. Alisimama na kufunga mlango. Kabla ya kutoka nje alisema: "Lusifa! Lusifa amekwishafanya roho yako kiti chake." Padri alionekana akitoka nje kasi sana

> na Biblia yake kwapani. Rosa alifunga mlango. Hakuzidi tena kumwona Padri kwa siku zilizofuata. (uk 48-49)

Katika dondoo hili tunaweza kujiuliza maswali kadhaa ya kiuchambuzi: Je, ni nani aliyeshindwa, Padri au Rosa? Je, njia aliyoitumia Padri katika kuanza mazungumzo yake na Rosa ilikuwaje?

Tukiyachunguza vizuri mazungumzo kati ya mhusika Padri na Rosa tunaweza kubaini kuwa Padri anaonesha udhaifu mkubwa kama mlezi wa kiroho katika maeneo makuu mawili:

Kwanza, mwanzo wa maongezi yake na Rosa si mzuri. Padri anaanza kwa maneno makali ambayo yanamfanya Rosa ashindwe kumsikiliza vizuri hata pale anapoanza kumsomea Biblia. Maneno kama vile “wewe maskini wa roho”, “ mwovu huoneka kwa matendo” ni maneno ambayo yanaonesha kuwa tayari mhusika Padri alikwishamuweka Rosa kwenye kizimba cha hukumu kama mtu mwovu. Kwa kuzingatia saikolojia ya mhusika Padri, yaani jinsi alivyo mkali, tunajiuliza ukali huu unasababishwa na nini? Tuonavyo sisi ukali wa mhusika Padri unawakilisha mtazamo na tabia ya viongozi wengi wa dini kupenda kupewa heshima na utii katika jamii na kuchukuliwa kama kipimo cha usahihi hata pale ambapo viongozi hao hawapo sahihi.

Pili, mhusika Padri anaonekana kukata tamaa juu ya Rosa. Kwa mtazamo wake anaona kuwa Rosa harekebishiki tena. Tukitumia kigezo cha yale anayoyasema mhusika Padri tunaweza kulithibitisha hili kupitia maneno yake. Mwandishi anasema,

> "Lusifa! Lusifa amekwishafanya roho yako kiti chake." (uk 49)

Hii ni hali ya kushindwa na kukata tamaa, jambo ambalo halitakiwi kwa mtu anayejiita mtumishi wa Mungu.

Jambo la tatu linalostahilli kutazamwa kwa undani ni ujasiri wa Rosa. Rosa alipata wapi ujasiri wa kumjibu Padri kwa maneno makali kiasi hicho? Katika maisha ya kawaida ni vigumu kukutana na mhusika kama Rosa ambaye angediriki kumchachafya Padri kiasi hicho. Katika jamii zetu mapadri wamepewa heshima ya hali ya juu kiasi kwamba kila kitu wakisemacho huchukuliwa kama kauli ya mwisho ambayo inahitaji utekelezaji pasipo maswali. Je, kwa kumpa Rosa ujasiri wa kumjibu Padri mwandishi anataka kuiambia nini jamii? Pengine iko haja ya kuhoji usahihi wa mamlaka za kidini.

Kwa upande mwingine mwandishi anaonyesha kuwa, kushindwa kwa Padri kutimiza jukumu lake kama mlezi wa kiroho kulichangia katika maangamizi ya Rosa. Hili tunaliona pale ambapo mhusika Rosa mwisho wa uhai wake anaonesha kuwa angetamani kuendelea kumsikiliza Padri. Mwandishi anasema,

> "Alianza sasa kuona nyotanyota machoni. Alipiga kelele.
> Padri! Ninamwona Padri! Unasoma nini! Biblia! Biblia!
> Padri! Padri! Usitoke nje! Ningoje! Niambie zaidi!" (uk 91)

Dondoo hili linatudhihirishia kuwa mwandishi anamtazama Padri kama yeye ndiye aliyeshindwa kutimiza wajibu wake kama mlezi wa kiroho. Kutokana na kushindwa kwa mhusika Padri, mhusika Rosa anaangamia. Tuonavyo sisi kushindwa kwa mhusika Padri kunaashiria kushindwa kwa mfumo mzima wa imani inayowakilishwa na mhusika huyo na hivyo matokeo yake ni uangamivu wa wale wote ambao wanamwamini mhusika huyo.

4.2.3.2 Mhusika Padri kama Kiongozi wa Ibada

Katika *Rosa Mistika*, mhusika Padri anabeba jukumu la kuongoza ibada ya mazishi ya marehemu Zakaria, Regina na Rosa. Hili ni jukumu la pili katika riwaya hii, ambalo linamdhihirisha mhusika Padri kama kiongozi wa kanisa katika jamii. Mwandishi anasema,

> Saa sita padri alifika kufanya ibada ya mazishi.
> Padri alipofika maiti walikuwa wamelazwa kanisani.
> Alivaa nguo na kuanza ibada.
> Alipofika kwenye maiti aliwanyunyizia maji ya
> baraka…(uk 94)
> Padri aliendelea na ibada . …… Padri alichukua sepetu
> Na kutupa udongo kidogo katika kila kaburi. (uk 95)

Katika dondoo hili tunamwona mhusika Padri akiufanya uhusika wake kama kiongozi wa ibada ya mazishi. Jukumu hili linaidhihirisha nafasi yake kama kiongozi wa kanisa katika jamii. Kwa hiyo, uchambuzi wetu wa mhusika Padri katika riwaya ya *Rosa Mistika* unaonesha kuwa mhusika Padri ni kiongozi wa kanisa katika majukumu yake mbalimbali ya kidini. Hata hivyo, tumeona kuwa mhusika Padri ameshindwa kutimiza baadhi ya majukumu yake hususan jukumu la malezi ya kiroho.

4.3 *Gamba la Nyoka*

4.3.1 Utangulizi

Riwaya ya *Gamba la Nyoka* iliandikwa na E. Kezilahabi na kuchapishwa mwaka 1979. Hii ni miongoni mwa riwaya tuliyoitumia kama data msingi katika utafiti wetu unaohusu usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Riwaya ya *Gamba la Nyoka* ni riwaya ambayo inaonyesha jinsi maamuzi ya kisiasa yaliyochukuliwa pasipo kutafakari yanavyoweza kuwa na madhara makubwa kwa wakulima wanyonge. Riwaya hii ina wahusika wengi kama vile: Mamboleo, Mambosasa, Padri Madevu, Padri Johnson, Mama Tinda, Tinda, Mkuu wa Wilaya na wengine wengi. Jukumu letu katika utafiti huu ni kuwachunguza wahusika wawili mapadri wanaojitokeza katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*.

4.3.2 Mhusika Padri katika *Gamba la Nyoka*

Katika riwaya ya *Gamba la Nyoka* tumeona kuwa mhusika Padri anaufanya uhusika wake akiwa kama kiongozi wa kanisa na mwanamume wa kawaida katika jamii. Akiwa kama kiongozi wa kanisa, Padri anashiriki katika matukio mbalimbali ya kikanisa kama vile kuungamisha waumini wake na kusoma misa. Uhusika wake kama mwanamume wa kawaida katika jamii unaonekana kupitia matendo na mawazo yake. Kwa mfano Padri kama mwanamume wa kawaida anafanya matendo kama vile: kuzini, kugombana na kupigana, uuaji, na kadhalika. Mwandishi anasema,

> Siku hiyo misa ya kwanza ilikuwa inasomwa na Padri
> 'Emptyhead', Mmarekani mmoja aliyejulikana sana kijijini
> kwa nyendo zake za chinichini kuhusu wake za watu…..
> wakristo walimwita Padri Madevu kwa sababu ya ndevu
> zake nyingi. Hili ndilo jina lililojulikana zaidi kijijini.

> Kabla ya kuanza, Padri Madevu alitupia macho upande
> wa wanawake; aliwaona wanawake fulani waliokuja kuungama
> dhambi zao juzi….Alizikumbuka:
> "Nilitembea na Padri Johnson mara nne." Padri Johnson
> alikuwa padri mwenzake katika parokia hiyo (uk 4)

Katika dondoo hili, mwandishi anatutambulisha kwa wahusika wawili ambao ni Padri Madevu na Padri Johnson. Jambo la pili linalojibainisha kupitia dondoo hili ni kabila au utaifa wa mhusika Padri. Tunaambiwa kuwa mhusika Padri Madevu ni Mmarekani. Pia tunaona kuwa tabia zao zinajibainisha wazi. Wote wawili wana tabia ya uzinzi. Dondoo hili linatupatia picha ya Padri kama kiongozi wa kanisa na mwanamume wa kawaida katika jamii. Jambo la kwanza analolifanya Padri Madevu kabla ya kuanza ibada ni kutazama upande wa wanawake. Kitendo hiki kinadokeza juu ya tabia yake ya kupenda ngono. Hapa pia tunaona kuwa mhusika Padri anawaza kama Padri na kama mwanamume wa kawaida katika jamii. Hebu sasa tuujadili uhusika wa mhusika Padri kwa mapana yake katika nafasi zake mbalimbali kama zinavyojitokeza kupitia matendo yake katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*. Uchunguzi wetu umemzingatia zaidi mhusika Padri Madevu kwa kuwa amejitokeza mara nyingi na matendo yake yanaonekana dhahiri.

4.3.2.1 Padri kama Kiongozi wa Kanisa katika Jamii

Kama tulivyokwishasema hapo juu, mhusika Padri anaufanya uhusika wake kama kiongozi wa kanisa katika jamii pale anaposhiriki katika matendo ya kuongoza ibada/misa. Mwandishi anasema,

> Kabla ya kuanza misa, Padri Madevu alitupia macho upande wa wanawake; aliwaona wanawake fulani waliokuja kuungama dhambi zao juzi. (uk 4)

Katika dondoo hili tunaona kuwa Padri ana jukumu la kuongoza misa pamoja na jukumu la kuwaungamisha waumini wake. Majukumu haya yanaonyesha uhusika wa mhusika Padri kama kiongozi wa Kanisa katika jamii. Katika jukumu lake kama kiongozi wa Kanisa katika jamii, mhusika Padri Madevu anaonekana pia akisoma Injili. Mwandishi anasema,

> "Injili ya Mtakatifu Luka yaendelea 21, 9-19". Padri Madevu alipiga kelele. Padri Madevu alipenda sana maandishi ya Luka. Kwake Luka alikuwa profesa kati ya mitume. (uk 60)

Katika dondoo hili tunamwona mhusika Padri akisoma injili. Jukumu hili linamfunua mhusika Padri kama kiongozi wa Kanisa katika jamii. Ifahamike kuwa, tunapozungumzia kuwa mhusika Padri anaufanya uhusika wake kama kiongozi wa Kanisa katika jamii, tunamhusisha Padri na matendo ambayo kwa kawaida katika jamii ambamo mapadri wamo, ni yeye (Padri) huyafanya.

4.3.2.2 Padri kama Mwanamume wa Kawaida katika Jamii

Kwa sehemu kubwa katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*, mhusika Padri anaonekana kujitokeza zaidi kama mwanamume wa kawaida katika jamii. Hili limejidhihirisha kupitia matendo ya mhusika Padri kama vile hasira, uzinzi, ugomvi, uuaji, uonevu, dharau, na uchochezi. Matendo yote haya ni matendo ambayo yanaweza kufanywa na mwanamume wa kawaida katika jamii. Kwa mfano, kama mwanamume wa kawaida katika jamii tunamwona mhusika Padri anahitaji kujamiiana. Mwandishi anatuonyesha kuwa mhusika Padri Madevu ana mahusiano ya kingono na muumini

wake Mama Tinda. Kutokana na miiko ya dhehebu lake Padri analazimika kutumia vidonge vya majira ili kuzuia ujauzito ambao unaweza kuleta aibu kwao. Mwandishi analionyesha hili katika ukurasa wa 7. Mwandishi anasema,

> "Watoto wamekwenda wapi?" aliuliza Padri Madevu.
> "Wamekwenda kucheza kwa majirani."
> "Leo nimekuletea tena vidonge vingine. Vile nafikiri vimekaribia kwisha," Padri Madevu alisema hali akifungua mkoba wake na kutoa hivyo vidonge.
> "Ukiendelea kumeza vidonge hivi hatutapata aibu ya aina yoyote…. Lazima tujitahidi kutunza heshima ya majina yetu." Padri Madevu alisema hali akimsogelea.
> "Hebu nikafunge mlango; Mama Tinda alisema akiinuka.(uk 7)

Jambo lililo dhahiri katika dondoo hili ni kuwa, mhusika Padri Madevu ana mahusiano ya kingono na Mama Tinda ambaye ni muumini wake. Jambo hili ni kinyume na maadili ya upadri. Kinachoonekana hapa ni kwamba mhusika Padri anajitahidi kushindana na vikwazo alivyowekewa na dini yake ambavyo havimruhusu kujamiiana. Kwa mtazamo wa mwandishi, upadri ni mzigo na unatakiwa kusahauliwa. Mwandishi analidokeza hili kupitia kwa mhusika Mama Tinda. Mwandishi anasema,

> "Padri, ulikuwa umesahau mzigo wako."
> "Huu si mzigo". Alisema Padri Madevu akicheka akiipokea alama yake ya upadri.
> "Upadri si mzigo?" aliuliza Mama Tinda kwa kejeli. Wakati huu Padri Madevu alikuwa akitafuta mahali pa kupachika hicho kimsalaba. (uk 7-8)

Katika dondoo hili, mwandishi anadokeza kuwa upadri ni mzigo kwani unamweka Padri katika katazo la kutojamiiana huku yeye mwenyewe akiwa anahitaji jambo hilo. Padri analazimika kuvunja miiko ya upadri kwa kufanya zinaa kwa siri. Padri Madevu anatumia upadri wake pamoja na zawadi mbalimbali kumrubuni Mama

Tinda. Inavyoonekana, Mama Tinda ameaminishwa kuwa uzinzi anaoufanya na Padri Madevu ni kitendo cha ukarimu kwa mtumishi wa Mungu. Mwandishi anasema,

> "Napika." Mama Tinda alisema sasa kwa macho yenye kurembuka. Picha ya Bikira Maria, saa ya mkono, na chupa ya marashi-Mungu ampe nini!
> "Napika," alisema tena hali wakiingia chumbani.
> Saa kumi na mbili. Padri Madevu alikuwa sasa amekaa tena kwenye kiti sebuleni. Mama Tinda alikuwa amepiga magoti mbele ya Padri Madevu.
> "Nipe baraka yako kabla hujaondoka."
> Padri Madevu ambaye alikuwa amekwishaaga mara ya pili, alisimama kwa utukufu. Alipanua mikono yake yote miwili, akakusanya upepo ulioweza kuzamisha karua ndogo zenye matanga makubwa, akasema bila kucheka,
> "Mungu akubariki kwa wema na ukarimu wako unaowafanyia watumishi wake." Kisha kwa mkono wake wa kulia alikatakata hewa. "Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu," alimalizia kwa sauti nzito ya kinabii. "Amina." Mama Tinda alijibu, bila kuulizwa, akiamini kuwa dhambi zake zote zilikuwa zimeondolewa. (uk 8-9)

Katika dondoo hili tunaona wazi kuwa mhusika Padri Madevu anafanya uzinzi na Mama Tinda kinyume na amri ya sita, katika mafundisho ya Kanisa Katoliki. Hapa tunaweza kujiuliza swali, inakuwaje kiongozi wa kiroho anayefundisha kuwa uzinzi ni dhambi kisha yeye azini? Ni dhahiri kuwa mhusika Padri Madevu ni mnafiki. Tabia hii ya Padri Madevu si nzuri na mwandishi kwa kupitia mhusika Tinda anaonesha kuwa anamchukia Padri Madevu kwa sababu ya tabia yake hii. Mwandishi anasema,

> "Naona nyayo za pikipiki ya Padri Madevu….
> Mama, mimi Padri Madevu simpendi!" (uk 11)

Hivyo tunaona kuwa mhusika Padri kwa kupitia tabia ya uzinzi, anaufanya uhusika wake kama mwanamume wa kawaida katika jamii.

Aidha, mhusika Padri anajitokeza kama mwanamume wa kawaida katika jamii kupitia tabia yake ya uchochezi. Mhusika Padri Madevu anaonekana kuwa mchochezi kupitia mahubiri yake. Mwandishi analionesha hili hasa katika sura ya saba ya riwaya yake. Mwandishi anasema,

> "Ndugu zangu Wakristo. Tazameni lakini msiseme, tesekeni msiseme. Naweza kusikia wazi mioyo yenu ikiambizana hivyo baada ya kimbunga kikali kilichopita. Ndugu zangu. Mioyo yenu ina mengi ya kusema lakini sasa imeinama kimya kama mihindi baada ya kusukumwa na upepo mkali. Tazameni! Shamba la Bwana lilikuwa kubwa lakini sasa limeingiliwa na ndege na nzige wa jangwani wenye njaa isiyomithilika. Tazameni wenyewe hamna haja ya kuambiwa! Vita vimetokea na damu imemwagika; mmerukaruka kichura ndugu zangu wapenzi; mmepigwa na mvua nje mkawa katika hali ya upweke; mmehamia Vibandani na kuacha nyumba zenu nzuri. Yesu mwenyewe alisema, 'Kabla ya hayo yote, watawakamateni na Kuwadhulumu.' Kwa hiyo Wakristo wapenzi vumilieni. Mungu atawapa makubwa mbinguni kuliko magari yao …Huu ndio mwanzo wa kuanguka kwa nchi yenu. Nawaambieni kweli! Maneno yangu mtayakumbuka nitakapokuwa nimekwenda!"
> ….Padri Madevu aliendelea na mafundisho yake. Watu walikuwa kimya. …..Mafundisho yaliyokuwa marefu siku hiyo na yote yalikashifu jitihada za serikali katika kuhudumia watu wake. (uk 61)

Katika dondoo hili tunaweza kuona kuwa kile kinachoonekana katika mafundisho ya Padri Madevu ni uchochezi wa kuwatia ugumu wananchi kuichukia serikali yao. Ni kutokana na mafundisho haya ya uchochezi na kukashifu serikali, ndipo vijana wawili, Mamboleo na Mambosasa wanaamua kumhoji Padri Madevu juu ya mafundisho yake. Matokeo yake mwandishi anatuonesha kuwa Padri Madevu anaonesha dharau kubwa kwa vijana hawa kwa kuwakaribisha mifupa (chakula cha mbwa). Kitendo hiki kinawakasirisha Mambosasa na Mamboleo jambo ambalo

linazua ugomvi unaowasababishia vijana hawa majeraha na maumivu makali. Mwandishi anasema,

> "Sasa nitawaletea zawadi muitakayo," alisema
> Padri Madevu akiinuka. Baada ya muda mfupi alirudi na sahani iliyokuwa imefunikwa kitambaa.
> Aliiweka sahani hiyo mezani, akakaa, kisha akasema, akiifunua: "Haya kuleni."
> Ndani ya sahani mifupa na makongoro ambayo hutumika kwa chakula cha mbwa yalikuwa yametuna.
> Ghafla Mambosasa alimrukia Padri Madevu akamkaba shingo. Alimpiga ngumi moja kali na Padri Madevu akaanguka kwa nyuma akiwa bado kwenye kiti chake….
> Lakini ghafla Padri Madevu alimrusha Mambosasa kwa mguu hadi mlangoni. Mambosasa aligonga kichwa chake mlangoni akaanguka chini. Akawa hana fahamu.
> Mamboleo alichukua kiti akampiga nacho Padri Madevu alipokuwa bado akijaribu kusimama. Padri Madevu alijitahidi akasimama akiwa ameshika chupa ya mvinyo aliyokuwa ameificha chini ya meza. Kwa chupa hiyo alimpiga Mamboleo kichwani akaanguka chini taabani.
> Padri Madevu aliwatazama Mambosasa na Mamboleo kwa dharau,… (uk 68-69)

Katika dondoo hili tunaona wazi kuwa mhusika Padri Madevu si tu kwamba ana dharau bali pia ana hasira na ni mgomvi. Tabia kama hizi ni tabia za mwanamume wa kawaida katika jamii kwani ni nadra kwa mtumishi wa Mungu kuwa na sifa kama hizi, kama yasemavyo maandiko matakatifu. Kwa mfano, tunaambiwa kuwa sifa mojawapo ya mtumishi wa Mungu ni kutokuwa mgomvi. Biblia inasema:

> Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi;
> bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye
> kufundisha, mvumilivu (2 Timotheo 2:24)

Pia, mhusika Padri anajitokeza kama mpinga mapinduzi. Mwandishi analisema hili kwa kuwapitia wahusika Mamboleo na Mambosasa. Wahusika hao wanasema,

> " Unafikiri kuwa kesho tukimshtaki kwa mkuu wa wilaya kwamba ni mpinga mapinduzi hataweza kufukuzwa nchini?" (uk 78)

Dondoo hili linaonesha wazi kuwa mwandishi anamwona mhusika Padri Madevu kama mpinga mapinduzi. Mahali pengine mwandishi anamwona mhusika Padri kama kikwazo cha maendeleo katika jamii. Mwandishi anasema,

> "Usinikumbushe habari za Padri Madevu!
> Alikuwa kama upanga wenye sumu kwa maisha ya kijiji hiki!
> Angekuwepo leo kijiji hiki kisingekuwa hivi. Tungekuwa sasa tunaitwa wasaliti wa nchi!" (uk 110)

Huu pia ni ushahidi mwingine wa uhusika wa Padri kama mwanamume wa kawaida katika jamii. Kwa upande mwingine tunaona kuwa mwandishi anaonesha kuwa mhusika Padri Madevu ana ubaya uliopitiliza. Mhusika Padri anaonekana kama mwuaji. Tukitumia kigezo cha yale ambayo wahusika wengine wanasema kumhusu mhusika Padri tunaweza kulithibitisha hili kupitia mazungumzo ya Mambosasa na Tinda. Mwandishi anasema,

> "Alikuwa msaliti wa nchi. Wewe mwenyewe unajua kuwa alipewa sumu na Padri Madevu ili aiweke kisimani! Naye alifanya hivyo akaua watu wengi! (uk 110)

Kupitia dondoo hili tunaweza kujiuliza ikiwa kweli inawezekana mtumishi wa Mungu kumpa mshirika wake sumu kwa ajili ya kuwaangamiza wanadamu wenzake. Tendo hili linaonesha kuwa mhusika Padri Madevu ni mwanaume wa kawaida na hayuko karibu na Mungu kama jamii inavyomwona.

Mwisho, tunamwona mhusika Padri kama mwanaume wa kawaida katika jamii, anajitokeza kama jasusi. Mwandishi anasema,

> "Pia iligunduliwa kwamba Padri Madevu hakuwa Padri. Alikuwa Profesa wa uchumi……

Padri Madevu alikuwa C.I.A. (uk 115)

Hapa tunamwona mhusika Padri akiufanya uhusika wake akiwa kama jasusi wa Kimarekani. Dondoo hili la mwisho linatuonesha kuwa upadri unaweza kutumiwa kama kichaka cha kujificha na kufanya maovu mengi katika jamii. Kwa upande mwingine tunaweza kusema kuwa mhusika Padri ni kiwakilishi cha ubepari na ukoloni mamboleo kutokana na tabia ya ujasusi.

Kwa hiyo, kutokana na uchambuzi wetu wa mhusika Padri katika *Gamba la Nyoka*, tunaona kuwa mwandishi anamwona Padri kama mwanamume wa kawaida na mtenda dhambi kama walivyo watenda dhambi wengine. Aidha tunaona kuwa mwandishi anamwona mhusika Padri kama mtu aliye na kiburi kutokana na madaraka yake ya kidini katika jamii.

4.4 *Nagona*

4.4.1 Utangulizi

Riwaya ya *Nagona* iliandikwa na E. Kezilahabi na kuchapishwa mwaka 1990. Hii ni riwaya mojawapo tuliyoitumia kama data msingi katika utafiti wetu. Katika riwaya hii, kuna mhusika jumui "Mimi" (wahusika wengi katika mmoja). Hata hivyo mhusika Padri anajitokeza pia katika riwaya hii kupitia mhusika jumui "mimi" na ndiye tunayemchunguza. Hapa chini tumeangalia sura mbalimbali za mhusika Padri katika *Nagona*.

4.4.2 Padri kama Mtu Mwenye Sauti katika Jamii

Katika *Nagona* mhusika Padri anajitokeza kama mtu mwenye sauti katika jamii. Tunaelezwa kuwa hakuna mtu mwingine mwenye uwezo wa kusema isipokuwa mhusika Padri na mzee mmoja. Mwandishi anasema,

> "Kwa nini hasemi?"
> "Nani?"
> "Yule mama."
> "Si yeye peke yake. Watu wa mji huu hawasemi.
> Anayezungumza katika mji huu ni mimi, na labda mzee mmoja karibu na mto.
> Sisi sote wawili tunaitwa vichaa katika mji huu. Wanatuona wendawazimu. Wakituona tu wanakimbia."
> "Kwa sababau mnazungumza!"
> "Kwa sababu hatujui kuzungumza."
> "Wao wanawasilianaje?"
> "Lugha waijuayo ni kimya."
> "Wanaelewana?"
> "Tena vizuri sana. Kwa muda wa karne sasa hapajatokea machafuko yoyote.
> "Hukupita kwenye msitu fulani?" (uk 8)

Katika dondoo hili hapa juu, tunaelezwa kuwa mhusika Padri ni mtu mwenye sauti katika jamii. Jambo hili linaashiria kuwa katika hali ya kawaida katika jamii zetu nyingi haswa maeneo ambayo Ukatoliki umeenea, mapadri ni watu wenye sauti. Chochote wakisemacho hutekelezwa pasipo maswali. Tunaweza kusema pia kwamba huenda mwandishi anaona kuwa uhuru wa kusema umehodhiwa na viongozi wa Kanisa Katoliki.

4.4.3 Padri kama Mtu Mwenye Uwezo Kuliko Wengine

Katika *Nagona* mhusika Padri ana chakula wakati wengine wote hawana. Tunaambiwa kuwa Padri anakula wakati wengine wanakula matumaini yao. Mwandishi anasema,

> “Watu mjini humu wanakula nini? Sioni mazao mahali popote!”
> “Hapa hawali chakula unachokielewa wewe.Ni mimi na yule mzee mtoni tulao na kunywa.
> “Nina shehena ya kututosheleza karne na karne.”
> “Wengine wanakula nini?”
> “Wanaishi kwa matumaini. Wanakula matumaini yao wenyewe ambayo wanasema huzaliana siku hadi siku.” (uk 9)

Katika dondoo hili tunadokezewa kuwa mhusika Padri na mzee ndio pekee wanaokula. Ikumbukwe kuwa mzee huyu hufika kutumikia misa Jumapili, kwa hiyo ni mtumishi kanisani. Dondoo hili linaashiria kuwa mhusika Padri ni mtu mwenye uwezo au utajiri. Tunaamini pia kwamba mhusika Padri ameupata uwezo huo au utajiri huo kutoka kwa watu walioko chini yake. Jambo hili linatufanya tuone kuwa mhusika Padri anawakilisha utabaka ulioasisiwa na wakoloni.

4.4.4 Padri kama Mwelekezaji (Mwonyesha Njia)

Katika *Nagona*, tunamwona mhusika Padri akijitokeza kama mtu anayeonyesha njia au mwelekezaji. Katika jukumu hili Padri anapaswa kuwaelekeza wengine njia wanayopaswa kuifuata ili wafike kule waendako. Hili tunaliona pale “mimi” anaposema kuwa Padri alimwonyesha njia ya kupita. Mwandishi anasema,

> Kesho yake asubuhi padri alinielekeza njia ya kufuata ili kumwona yule mzee aliyenielezea hakuwa mbali sana na mji. (uk 11)

Dondoo hili linatuthibitishia kuwa Padri ana kazi ya kuwaonyesha wengine njia. Pengine kuonyesha njia huko kunaweza kuchukuliwa kama nafasi ya kuwaongoza wengine katika kuifikia kweli.

4.4.5 Padri kama Mlevi katika Jamii

Katika *Nagona* tunamwona Padri akiufanya uhusika wake kama mlevi. Tunaambiwa kuwa Padri anakunywa pombe usiku na mchana. Kitendo cha kunywa pombe usiku na mchana kinaashiria kuwa padri ni mlevi. Mwandishi anasema,

> "Subiri nikafunge mlango."
> Alipofunga mlango nilimwona akifungua kabati ambamo alitoa chupa moja inayoelekea kuwa kinywaji cha pombe. Aliiweka mezani, halafu akatoa glasi mbili. Alimimina kinywaji kilichoelekea kuwa mvinyo.
> "Kunywa. Najua una kiu," alisema.
> "Naweza kupata maji kwanza?" ….
> " Wewe nani?" nilimwuliza
> "Mimi ni padri wa mji huu. … (uk 6,7)

Katika dondoo hili tunamwona mhusika Padri kama mlevi. "Mimi" anapomtembelea Padri, kitu cha kwanza anachokaribishwa ni mvinyo. Hili pia tunaliona katika ukurasa wa 13. Mwandishi anasema,

> "Ndiyo. Hukukutana na padri huko mjini? Bila shaka Yeye ndiye amekuelekeza nilipo. Tupo vichaa wawili tu hapa. Yeye na mimi, ingawa nafikiri kichaa chake kimezidi."
> "Kwa nini unafikiri hivyo?"
> "Anakunywa usiku na mchana. Mimi sifanyi hivyo…(uk13)

Dondoo hili linaonesha kuwa mhusika Padri ni mlevi. Hapa tunaweza kujiuliza swali: Kwa nini Padri anakunywa pombe usiku na mchana? Tuonavyo sisi mhusika Padri hanywi pombe kwa sababu ya starehe bali mwandishi anautumia ulevi wa mhusika Padri kudokeza hali ya kuchanganyikiwa na kukata tamaa. Jambo hili limejadiliwa katika kipengele cha mjadala wa matokeo ya utafiti.

4.4.6 Padri kama Mtu asiye na Heshima kwa Wazee

Katika *Nagona* tunamwona mhusika Padri akijitokeza kama mtu asiye na heshima kwa wazee. Hili linaonekana pale ambapo Padri anawakuta wazee wamekaa na badala ya kuwaamkia anasubiri kupokea salamu kutoka kwao. Mwandishi anasema,

> Alipoketi kulikuwa na muda wa kimya, halafu babu, akimwangalia padri usoni, aliuliza,
> "Tumejuliana hali?" Padri alikaa kimya.
> Wazee wote walimtazama.
> "Je, ulitarajia sisi sote hapa tukusalimu wewe kwanza? Hata mchawi hubisha hodi."
> Padri alitabasamu. Aliwatazama wazee halafu akafungua kinywa chake. "Hakuna mkristo miongoni mwenu?" (uk 17)

Katika dondoo hili tunaona kuwa Padri amekosa heshima kwa wazee. Katika hali ya kawaida, inatazamiwa kuwa mtu akiwakuta watu mahali fulani aanze yeye kuwasalimia. Kinyume chake tunaona kuwa Padri hafanyi hivyo ingawa ndiye aliyewakuta wazee. Je, hapa tunajifunza nini? Kwamba Padri analazimisha heshima kutoka kwa wale anaowaongoza? Ni kwa nini Padri anauliza "hakuna mkristo miongoni mwenu?" Tuonavyo sisi mwandishi anakusudia kuionyesha jamii kuwa Padri kutokana na cheo chake katika dhehebu analoliongoza, anategemea kupokea heshima kutoka kwa watu wa rika zote lakini yeye haitoi heshima hiyo kwa yeyote.

4.4.7 Padri kama Binadamu wa Kawaida

Mhusika Padri anaidhihirisha tabia yake kama binadamu wa kawaida. Kama binadamu wa kawaida, Padri anakasirika, anatukana na kadhalika. Mwandishi anasema,

> "Sasa kwa nini uko hapa basi? Unafanya nini hapa?
> Baradhuli! Nafikiri unaungama kumbe unafanya mchezo! Unaweza kunihadaa mimi lakini huwezi kumhadaa Yeye aliye mbinguni!"

> “Ndiyo maana niko hapa.”
> “Hayawani! Juha! Jinga! Pumbavu!”
> “Mimi ni baradhuli, juha, hayawani, jinga pumbavu. Baba, unanitukana?”
> “Samahani! Mimi pia ni binadamu…. (uk 91,92)

Katika dondoo hili tunamwona mhusika Padri amekosa uvumilivu kutokana na ukubwa wa dhambi za “mimi” ambapo anamtukana. Pia Padri anakiri kuwa yeye ni binadamu wa kawaida. Kama binadamu wa kawaida anaweza kukosea. Swali linakuja: ikiwa Padri ni binadamu wa kawaida na anaweza kutenda dhambi kama wanavyotenda wengine, ni kweli anao uwezo wa kuondoa dhambi kama waumini wake wanavyoamini? Hili tutalijadili baadaye katika swali linalohusiana na dhamira zinazowakiliswa kupitia mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi.

4.5 Dhamira Zinazowasilishwa na Mhusika Padri

4.5.1 Utangulizi

Katika utafiti huu, tumeangalia mawazo mbali mbali yanayowasilishwa kupitia mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Kwa kupitia mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi tumeweza kubaini dhamira kadhaa zinawasilishwa na mhusika huyo kama tulivyozijadili hapa chini.

4.5.2 Suala la Malezi ya Kiroho

Dhamira ya malezi ya kiroho inajitokeza kwa sehemu kubwa katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Malezi ya kiroho hapa tunamaanisha mafunzo ya kiroho apewayo mtu kwa lengo la kumsaidia kukabiliana na maisha na kumfanya awe na uadilifu unaotakiwa katika jamii. Dhamira ya malezi kwa ujumla ndiyo inayotawala katika riwaya ya

Rosa Mistika. Dhamira ya malezi ya kiroho inawasilishwa na mhusika Padri pale anapotumwa kumwonyesha Rosa mwanga wa wokovu.

Mlezi ni mtu anayemtunza, kumhudumia na kumfundisha mtoto mpaka akue (K.K.S 2004:260). Tunamwona Padri akiwa na jukumu hili la kumfundisha Rosa. Mwandishi anasema,

> "Rosa, nimekuja kukusaidia; nimekuja kukuonyesha tena mwanga wa wokovu." (uk 48)

Katika dondoo hili tunaona kuwa mhusika Padri anaeleza kusudio lake la kwenda kumwona Rosa 'kumwonyesha mwanga wa wokovu'. Hapa Padri alikuwa akimaanisha kuwa amekwenda kwa lengo la kumpatia Rosa mafundisho ya kiroho. Fundisho mojawapo Padri analomfundisha Rosa ni kutokukata tamaa. Mwandishi anasema,

> "…Padri alifungua Biblia yake. Alianza kumhubiria Rosa:
> "Usikate tamaa. Rosa usikate tamaa."(uk 48)

Dondoo hili linatuonesha Padri akimfundisha Rosa asikate tamaa. Hata hivyo, tunaona kuwa pamoja na Padri kumfundisha Rosa asikate tamaa, tunamwona Padri akikata tamaa kwa kuona kuwa Rosa hafai tena. Mwandishi anasema,

> "Lusifa! Lusifa amekwishafanya roho yako kiti chake."
> Padri alionekana akitoka nje kasi sana na Biblia yake kwapani.
> Rosa alifunga mlango. Hakuzidi tena kumwona Padri huyo kwa siku zilizofuata. (uk 49)

Dondoo hili linaonesha kuwa Padri amekata tamaa kuendelea kumlea Rosa kiroho. Pengine kukata tamaa kwa Padri ndiko kulikochangia kuangamia kwa Rosa. Mwandishi anatudokezea hili kupitia kwa mhusika Rosa katika hatua za mwisho za uhai wake. Mwandishi anasema,

> “Alianza sasa kuona nyotanyota machoni.Alipiga kelele.
> “Padri! Ninamwona Padri!
> Unasoma nini! Biblia! Biblia! Padri! Padri!
> Usitoke nje! Ningoje! Niambie zaidi!” (uk 91)

Dondoo hili ni ushahidi tosha unaotuwezesha kuhitimisha kwamba mhusika Padri ameshindwa kutimiza jukumu la kutoa malezi ya kiroho na matokeo yake amechangia kwa namna moja au nyingine kuangamia kwa Rosa.

4.5.3 Unafiki wa Viongozi wa Kanisa Katoliki

Unafiki ni hali ya kujifanya kuwa ni rafiki hali ni adui; hali ya kutokuwa mkweli (K.K.S 2004:435). Dhamira ya unafiki inajitokeza kwa sehemu kubwa sana katika *Gamba la Nyoka*. Hata hivyo, dhamira hii tunaona imeanzia katika *Rosa Mistika* ingawa si kwa namna ya wazi bali kwa kudokezwa tu. Kitendo cha mhusika Padri kumfundisha Rosa asikate tamaa, kisha yeye (Padri) akakata tamaa, kinadokeza unafiki wa viongozi wengi wa dini ambao huwaelekeza waumini wao kufanya mambo ambayo wenyewe hawayafanyi. Mwandishi anasema,

> “…Padri alifungua Biblia yake. Alianza kumhubiria Rosa:
> “Usikate tamaa. Rosa usikate tamaa.” (uk 48)

> “Lusifa! Lusifa amekwishafanya roho yako kiti chake.”
> Padri alionekana akitoka nje kasi sana na Biblia yake kwapani.
> Rosa alifunga mlango. Hakuzidi tena kumwona Padri huyo kwa siku zilizofuata. (uk 49)

Tukiyachunguza madondoo hayo mawili hapo juu tunagundua kuwa mhusika Padri ni mnafiki. Anafundisha kutokukata tamaa lakini yeye anakata tamaa.

Katika *Gamba la Nyoka*, tunaona dhamira ya unafiki ikijitokeza kwa kiwango cha juu kupitia kwa mhusika Padri Madevu. Padri Madevu anafanya uzinzi na Mama Tinda chumbani na wanaporudi sebuleni Mama Tinda anamwomba Padri ampe baraka kabla hajaondoka. Mwandishi anasema,

> "Napika," alisema tena hali wakiingia chumbani.
> Saa kumi na mbili. Padri Madevu alikuwa sasa amekaa tena kwenye kiti sebuleni. Mama Tinda alikuwa amepiga magoti mbele ya Padri Madevu.
> "Nipe baraka yako kabla hujaondoka."
> Padri Madevu ambaye alikuwa amekwishaaga mara ya pili, alisimama kwa utukufu. Alipanua mikono yake yote miwili, akakusanya upepo ulioweza kuzamisha karua ndogo zenye matanga makubwa, akasema bila kucheka, "Mungu akubariki kwa wema na ukarimu wako unaowafanyia watumishi wake. Kisha kwa mkono wake wa kulia alikatakata hewa. "Kwa jina la Baba na la Mwana, na la Roho Mtakatifu," alimalizia
> Kwa sauti nzito ya kinabii. "Amina," Mama Tinda alijibu, bila kuulizwa, akiamini dhambi zake zote zilikuwa zimeondolewa. (uk 8-9)

Dondoo hili linatuonesha unafiki wa hali ya juu. Inakuwaje kiongozi wa dini anayefundisha kuwa uzinzi ni dhambi halafu yeye mwenyewe ni mzinzi? Mama Tinda anaonekana pia kuwa ameaminishwa na huyo kiongozi wake wa dini kuwa uzinzi wanaoufanya si dhambi bali ni kitendo cha ukarimu kwa watumishi wa Mungu, jambo ambalo si kweli. Ni dhahiri kuwa Padri Madevu ni mnafiki na anawakilisha viongozi wengine wa dini wanaotumia nafasi yao ya kuwa viongozi wa dini, kufanya uchafu wao chini ya mwamvuli wa uongozi wa dini. Swali la kujiuliza hapa ni je, unafiki wa Padri Madevu unatokana na asasi ya dini anayoiwakilisha au unatokana na utashi wake binafsi? Mwandishi anaonesha kuwa viongozi wa dini kama Padri Madevu ni wanafiki wakubwa na hawapaswi kuendelea kuishi katika jamii. Hili tunaliona pale ambapo dhambi ya uzinzi inawafikisha Padri Madevu na

Mama Tinda katika umauti, hivyo kutimiza ule msemo wa inzi kufia kwenye kidonda. Mwandishi anasema,

> "Ilikuwa baada ya polisi kufika ilipogunduliwa kuwa nyumbani kwa Mama Tinda kulikuwa pia na kilio. Mama Tinda na Padri Madevu walikuwa wamekauka hali wamekumbatiana." (uk 97)

Dondoo hili ni ushahidi kuwa dhambi ya unafiki, hatimaye inayachukua maisha ya Padri Madevu. Mwandishi anachotuonesha hapa ni kwamba viongozi wa dini wanafiki kama alivyo Padri Madevu mwisho wao hautakuwa mzuri. Wanaweza kufanya dhambi ya zinaa kwa kificho lakini kuna siku moja dhambi hiyo itakuwa dhahiri mbele ya macho ya mashahidi wengi. Hili ndilo lililotokea kwa Padri Madevu.

4.5.4 Uonevu na Kukosekana kwa Haki

Dhamira ya uonevu ni suala jingine ambalo linajitokeza kupitia mhusika Padri. Dhamira hii inajitokeza katika riwaya ya *Gamba la Nyoka*. Mwandishi anaonesha kuwa mhusika Padri ni mtu anayetumia nafasi yake vibaya kuwadhulumu na kuwaonea wengine. Hili linajidhihirisha kupitia adhabu ambayo vijana wawili Mambosasa na Mamboleo walipewa pasipo hata kusikilizwa. Hukumu ya kuchapwa viboko inayotolewa kwa vijana hawa inaonekana kufurahiwa na Padri Madevu huku akijua wazi kuwa ndiye aliyewapiga Mamboleo na Mambosasa. Mwandishi anasema,

> "Hawa vijana wamefanya kosa kubwa. Lakini tumewaonea huruma. Tumewapa adhabu ndogo tu.
> Ebu wachape viboko vitano vitano! Bila kuchelewa afande Matiko aliwaamrisha kulala chini. Akaanza kazi yake. Walijikaza kwa viboko viwili vya kwanza, vilivyofuata walikuwa wakipiga

> kelele kwa maumivu. Wakati wote huu Padri Madevu alikuwa akitingisha kichwa chake kwa furaha. (uk 83)

Dondoo hili linaonesha kuwa Padri Madevu anafurahia uonevu jambo ambalo si sahihi kufanywa na kiongozi na hasa kiongozi wa kidini. Mambosasa na Mamboleo wananyimwa haki. Hawakupata hata nafasi ya kumshitaki Padri Madevu. Mwandishi anasema,

> "Hatukupata hata nafasi ya kumshitaki Padri Madevu"
> "Mimi matako yanauma sana!" (uk 83)

Dondoo hili linaonesha kuwa mhusika Padri pengine kutokana na nafasi aliyo nayo anapewa upendeleo zaidi na hivyo wengine kunyimwa haki yao ya kisheria. Huku ni kukosekana kwa haki.

4.5.5 Suala la Uwezo wa Padri kuondoa Dhambi

Katika riwaya za Kezilahabi dhamira hii inajitokeza. Aidha, mwandishi anasaili uwezo wa Padri kuondoa dhambi huku yeye mwenyewe (Padri) akizitenda dhambi hizo. Dhamira hii inajitokeza katika *Gamba la Nyoka* na katika *Nagona*. Kwa mfano katika *Gamba la Nyoka* ukurasa wa 116 mhusika Tinda anasema,

> "Basi kama ni hivyo mimi nitakwenda motoni.
> Dhambi zote zile nilizoungama kwake bado hazijatoka!
> Zingine nimekwishazisahau!"

Dondoo hili linaonesha kuwa mhusika anasaili uwezo wa Padri kuondoa dhambi. Dhamira hii inajitokeza kwa uwazi zaidi katika riwaya ya *Nagona* pale mhusika Mimi anapohojiana na roho yake juu ya kitu kiwezacho kuisafisha. Mwandishi anasema,

> “Dawa gani iwezayo kukusafisha?”
> “Sisafishiki kwa chochote kile binadamu awezacho kukifikia.”
> “Lakini niliungama dhambi zangu zote.
> Dhambi za karne na karne. Nilikiri makosa yangu!”
> “Najua. Lakini ulipoteza muda wako. Hukusamehewa hata dhambi moja.”
> “Kwa nini?”
> “Uliungama kwa Padri mlevi.
> Watu kama hao huwa hawasikilizwi.
> Baraka zao huishia katika kufukuza tu nzi nyusoni pao.”
> “Lakini mimi binafsi nilikiri makosa yangu. Hiyo inatosha, Padri si ni kiunganishi tu?”
> “Uzushi! Hoja ilikuwa kubadili vitendo vyako na fikra zako kulingana na umri wa mtoto wetu.”
> “Mtoto wetu.”
> “Ndiyo. Mtoto wetu Dhamiri. Yeye, mimi na wewe tu kitu kimoja.
> Nilimtuma akukanye lakini hukumsikiliza ukidai yeye ni zao la jamii na uozo wake.
> Sisi sote tukaoza na jamii.” (uk 28-29)

Dondoo hili linaonesha kuwa Padri hana uwezo wa kuondoa dhambi kwa sababu yeye ni mtenda dhambi. Hapa tunaambiwa kuwa dhambi za “Mimi” hazikuondolewa kwa sababu aliungama kwa Padri mlevi na kwamba watu kama Padri huyo hawasikilizwi na Mungu. Mwandishi pia anasema kuwa baraka za Padri ambaye ni mlevi huishia katika kufukuza nzi nyusoni pao. Hapa tunaona kuwa neno nzi limetumika hapa kuwakilisha uchafu. Kama tujuavyo, nzi ni mdudu mchafu katika jamii zetu na ambaye hatakiwi kwani anaweza kuleta kipindipindu. Mwandishi anaona kuwa watu wanapoteza muda wao kwa kwenda kuungama kwa Padri wakati Padri naye ni binadamu mwenye dhambi.

4.6 Motifu Inayojitokeza kupitia Mhusika Padri

4.6.1 Utangulizi

Nkinde (2011:2), anamnukuu Mulokozi (2009) mbapo anasema, “Motifu ni kipengele radidi cha kijadi/kikaida au kimaudhui kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Mulokozi anatoa mifano ya motifu za kifasihi kuwa ni: motifu ya mama wa kambo, motifu ya safari, motifu ya msako, motifu ya mwanamke mshawishi, motifu ya bi kizee, motifu ya mzungu mweusi, motifu ya mtoto wa ajabu, motifu ya mtoto kigego, motifu ya mnyonge anayemshinda mwenye nguvu, motifu ya nunda/zimwi mla watu, motifu ya mwali aliyekataa kuolewa pia motifu ya taksiri (*Achille’s heel*)”.

Kwa mujibu wa Wikipedia The Free Encyclopedia (2013), “motifu (katika hadithi) ni kipengele chochote kinachojirudiarudia katika hadithi ambacho kina umuhimu wa kiishara.” (tafsiri yetu)

Hivyo basi, sisi katika utafiti wetu tumeangalia vipengele ambavyo ni radidi na vinavyohusiana na mhusika Padri ili kubaini iwapo kuna motifu yoyote inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Vipengele ambavyo tumeviangalia ni uradidi wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi hali kadhalika uradidi wa mawazo au dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi na uhusiano wake.

4.6.2 Motifu ya Padri Aliyeshindwa

Katika uchunguzi wetu wa riwaya teule ambazo ni *Rosa Mistika*, *Gamba la Nyoka* na *Nagona* tumeona kuwa motifu ya Padri aliyeshindwa inajitokeza kwa kiasi kikubwa sana. Tumeiita motifu ya Padri aliyeshindwa kwa kuzingatia kuwa mhusika Padri amerudiwa mara nyingi katika kazi za Kezilahabi akiwakilisha kushindwa. Kwa upande mwingine pia tumeona dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri nazo zinahusiana kwa namna moja au nyingine nazo zinaashiria kushindwa kwa mhusika Padri kwa njia moja au nyingine. Aidha, tumebaini kuwa motifu ya Padri aliyeshindwa katika riwaya za Kezilahabi inajitokeza kwa namna kuu mbili katika riwaya zote tatu tulizozichunguza.

Mosi, mhusika Padri ameshindwa kusimamia mafundisho yake/kauli zake. Kwa mfano, katika *Rosa Mistika* tunamwona Padri akimfundisha Rosa asikate tamaa, na kwamba kukata tamaa ni dhambi isiyosameheka. Jambo la kushangaza, Padri ndiye anayekuwa wa kwanza kukata tamaa juu ya Rosa kwa kuona kuwa tayari moyo wa Rosa umekaliwa na Ibilisi na ni vigumu kumrejeza upya. Mwandishi anasema,

> Padri alifunga Biblia yake. Alianza kumhubiria Rosa:
> “Usikate tamaa. Rosa usikate tamaa. Kukata tamaa ni dhambi isiyoweza kuondolewa hapa duniani.
> …….Kabla kutoka nje alisema, “Lusifa! Lusifa amekwishafanya roho yako kiti chake.” Padri alionekana akitoka nje kwa kasi sana na Biblia yake kwapani. Rosa alifunga mlango. Hakuzidi tena kumwona Padri huyo kwa siku zilizofuata. (uk 49)

Dondoo hili linaonesha kuwa mhusika Padri ameshindwa kuonesha msimamo katika kile anachokiamini kwa kukata tamaa. Kitendo cha Padri kutokuonekana tena kinaashiria kukata tamaa.

Pili, mhusika Padri ameshindwa kimaadili. Tukizichunguza riwaya mbili za *Gamba la Nyoka* na *Nagona* tunaona kuwa dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri zinaashiria kushindwa kimaadili. Kwa mfano katika *Gamba la Nyoka*, Padri ni mzinzi, mtukanaji, mgovi, mlevi na ana tabia nyingine ambazo hazipaswi kufanywa na kiongozi wa kiroho. Kwa mfano, katika *Gamba la Nyoka* tunaona kuwa Padri anafanya uzinzi na Mama Tinda na ili kuzuia mimba anamletea Mama Tinda vidonge vya kupanga uzazi. Mwandishi anasema,

> "Leo nimekuletea tena vidonge vingine. Vile nafikiri vimekaribia kwisha," Padri Madevu alisema hali akifungua mkoba wake na kutoa hivyo vidonge.
> "Ukiendelea kumeza vidonge hivi hatutapata aibu ya aina yoyote….Lazima tujitahidi kutunza heshima ya majina yetu." Padri Madevu alisema hali akimsogelea.
> "Hebu nikafunge mlango," Mama Tinda alisema akiinuka.
> (uk 7)

Dondoo hili linaonesha kuwa mhusika Padri anafanya zinaa huku akijua wazi kuwa kitendo hicho ni cha aibu. Aidha, dondoo hili linaonesha wazi kuwa mhusika Padri anajua kabisa kuwa kitendo anachokifanya ni kinyume na maadili na ndio maana anaamua kumletea Mama Tinda dawa za majira ili kuepuka aibu ambayo inaweza kuwapata iwapo mimba itatokea. Tunaweza kusema pia kwamba kutokana na dondoo hili mwandishi anamwona mhusika Padri kama "padri jina tu." Jambo hili linaashiria kuwa mhusika Padri hana utukufu wowote kama jamii inavyomwona. Kama Padri ni jina tu, maana yake tuonavyo sisi ni kwamba hana umuhimu wowote

katika jamii na dini yake anayoiwakilisha katika jamii haina umuhimu wowote na kwamba wanaomfuata ama wamepotea au hawaendi popote.

Aidha, tunaona pia kwamba Padri ni mtukanaji, jambo ambalo ni kinyume na maadili si tu ya upadri bali maadili ya jamii nzima kwa ujumla. Kwa mfano katika *Gamba la Nyoka* tunamwona Padri Madevu anagombana na vijana wawili Mambosasa na Mamboleo na anawapiga na kuwatukana. Mwandishi anasema,

> Padri Madevu aliwatazama Mambosasa na Mamboleo kwa dharau, akasema*: "Socialist garbage!"* (uk 69)

Dondoo hili linaonesha kuwa Padri Madevu ni mgomvi na mtukanaji jambo ambalo ni kinyume na maadili. Huu ni ushahidi kuwa Padri ameshindwa kimaadili. Hali kama hii inaonekana pia katika *Nagona* ambapo tunamwona Padri anamtukana mhusika "Mimi" wakati wa kumuungamisha. Mwandishi anasema,

> Baradhuli! Nafikiri unaungama kumbe unafanya mchezo! …Hayawani! Juha! Jinga! Pumbavu!
> "Mimi ni baradhuli, juha, hayawani, jinga, pumbavu, Baba unanitukana?" (uk 91-92)

Dondoo hili pia linaonesha kuwa mhusika Padri ameshindwa kimaadili kutokana na kuwa mtukanaji kinyume na maadili ya jamii na nafasi aliyo nayo katika jamii. Aidha, tunaona mhusika Padri ni mlevi jambo ambalo ni kinyume na maadili ya jamii na maadili ya uongozi, haswa uongozi wa kiroho. Hili linajitokeza katika *Nagona*. "Mimi" anasema,

> "Lakini niliungama dhambi zangu zote. Dhambi za karne na karne. Nilikiri makosa yangu!"
> "Najua. Lakini ulipoteza muda wako. Hukusamehewa hata dhambi moja."
> "Kwa nini?"

> “Uliungama kwa padri mlevi. Watu kama hao huwa hawasikilizwi. Baraka zao huishia katika kufukuza tu nzi nyusoni pao.” (uk 28-28)

Dondoo hili linaonesha kuwa mhusika Padri ameshindwa kimaadili kutokana na ulevi na kwamba kwa sababu hiyo Mungu hawezi kumsikiliza. Aidha katika dondoo hili, mwandishi anatuashiria kuwa Padri kutokana na yeye mwenyewe kuwa mlevi anapoteza nafsi za watu kwani wengi huenda kuungama kwake wakiamini kuwa dhambi zao zimeondolewa pasipo kujua kuwa Mungu hamsikilizi Padri huyo.

4.6.3 Mhusika wa Kimotifu (Mhusika Anayewakilisha Motifu)

Mhusika Padri kutokana na uradidi wake katika kazi za Kezilahabi na pia kutokana na uradidi na/au uhusinano wa dhamira nyingi zinazowasilishwa na mhusika huyo, tunaweza kusema kuwa Padri ni **mhusika wa kimotifu** katika kazi za Kezilahabi. Kama tulivyoona mhusika Padri anawakilisha **motifu ya padri aliyeshindwa,** kwanza kutokana na uradidi wake katika kazi nyingi za Kezilahabi, na pili kutokana na uradidi au uhusiano au mfanano wa dhamira zinazowasilishwa na mhusika huyo.

Hivyo basi, mhusika Padri si mhusika wa kawaida kama vile ambavyo wengine wangedhani bali ni mhusika wa kimotifu (*motifal character*). Pengine hii ni aina mpya ya mhusika katika fasihi kwa ujumla na fasihi ya Kiswahili. Tunaweza kuendelea mbele zaidi na kumfasili mhusika wa kimotifu kama mhusika anayejitokeza zaidi ya mara mbili katika kazi mbalimbali za mwandishi yuleyule, akiwakilisha dhamira radidi au zinazokaribiana au zinazohusiana na hatimaye kutokeza motifu ya aina fulani katika kazi hizo.

Tukizichunguza riwaya za Kezilahabi tulizozitumia kama data msingi, tunaona kuwa mhusika Padri anayejitokeza katika riwaya hizi anakidhi vigezo hivyo tulivyovitaja. Mhusika Padri anajitokeza katika *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990).

Aidha, tunaona pia kwamba dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya zote tulizozitumia katika utafiti wetu zinahusiana kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, katika *Rosa Mistika* tunaona dhamira ya unafiki inajitokeza na kuendelezwa katika *Gamba la Nyoka*. Dhamira nyingine kama vile ugomvi, ulevi, matusi, uonevu, suala la uwezo wa Padri kuondoa dhambi, n.k. zote tunaona zinahusiana kwani zinaonesha kuwa mhusika Padri hana maadili yanayohitajika, hivyo ameshindwa kama kiongozi wa kiroho na kama mwakilishi wa asasi ya dini anayoiwakilisha. Kwa hiyo, mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi ni mhusika wa kimotifu kifani na kimaudhui.

4.7 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

4.7.1 Mhusika Padri Anavyoelezewa katika Riwaya za Kezilahabi

Swali la kwanza katika utafiti wetu lilitaka kujua tunaweza kumchambuaje mhusika Padri na uhusika wake katika riwaya teule? Tumeona mhusika Padri amejitokeza katika sura mbalimbali. Kwa mfano katika *Rosa Mistika* tumeona kuwa Padri anajitokeza kama kiongozi wa kanisa katika jamii ambapo anatekeleza jukumu la kutoa malezi ya kiroho na kuongoza ibada ya mazishi. Tumeona hata hivyo kuwa mhusika Padri ameshindwa kumlea kiroho mhusika Rosa. Maswali ya kujiuliza hapa ni: kwa nini ameshindwa? Hali halisi katika jamii ikoje? Katika hali halisi haswa

katika jamii ambamo dini Katoliki inapatikana Padri hufanya shughuli hizi zinazojitokeza katika *Rosa Mistika*. Kushindwa kwa mhusika Padri kunaashiria nini? Nini kitatokea iwapo yule anayetoa malezi ya kiroho atashindwa? Jibu la maswali haya liko katika kile kilichompata mhusika Rosa. Kifo!

Kwa upande mwingine, kwa maoni yetu, tunaona kuwa kushindwa kwa mhusika Padri kunaashiria pia kushindwa kwa mfumo wa asasi ya kidini anayoiwakilisha, hususan, katika kuyaishi maadili yanayohubiriwa na viongozi wa dini hiyo na hivyo kushindwa kuwa kielelezo cha kuigwa kivitendo na waumini wao.

Pia tumeona kuwa mhusika Padri amejitokeza kama mwanamume wa kawaida katika jamii. Kama mwanamume wa kawaida Padri ni mzinzi, mgomvi, muonevu, mchochezi na ana dharau. Jambo tunalopaswa kulitazama hapa ni iwapo tunaweza kukutana kihalisi na mhusika mwenye matendo kama ya mhusika Padri katika jamii. Kihalisi wahusika kama Padri Madevu ambao wanazini na waumini wao wapo katika jamii zetu. Kwa mfano katika gazeti la *Risasi* la Jumamosi, Mei 4-7,2013, katika ukurasa wa mbele kuna kichwa, “Fumanizi la Padri: Kanisa Katoliki Latikisika.” Gazeti hili linaeleza habari za Padri mmoja aliyefumaniwa na mke wa mtu huko Marangu, wilaya ya Moshi Vijijini mkoani Kilimanajaro.

Aaidha, tunaamini huenda mwandishi alikutana kihalisi au aliwahi kuwaona wahusika wenye tabia anazozitaja katika riwaya zake. Katika mahojiano tuliyofanya na mwandishi, alipoulizwa juu ya msukumo wa ndani uliomfanya kuandika alisema hivi,

> "Msukumo wa ndani ni ngumu kidogo-kwa sababu mtu mwenyewe bado anaishi ambaye alinikasirisha-siwezi kutaja" (Mahojiano na Mwandishi, Mei, 24,2013, saa 7 mchana)

Kauli hii inaonyesha kuwa kuna tukio halisi lililotokea katika maisha ya mwandishi na ambalo lilimsukuma kuandika . Suala la huyo aliyemkasirisha ni nani halina umuhimu sana kwetu. Sisi tunaona kuwa mwandishi alikutana kihalisi na Padri au mapadri waliomkasirisha kutokana na tabia na mwenendo wao wa kinafiki na hatimaye akapata msukumo wa kuandika kuwahusu ingawa jibu la ni nani hasa aliyemkasirisha analo mwandishi mwenyewe.

Katika *Nagona* tumeona mhusika Padri amejitokeza katika nafasi mbalimbali. Kwanza, kama mtu mwenye sauti katika jamii. Katika jamii nyingi Padri anaheshimika sana na husikilizwa na wengi. Je, mwandishi alikuwa na lengo la kuonesha kuwa Kanisa Katoliki limehodhi sauti ya watu na kuwanyamazisha? Je, sauti ya Padri inawakilisha nini? Kwa upande wetu tunaamini pengine hili linaashiria uwezo wa kifedha na kadhalika walio nao mapadri katika jamii zetu.

Padri pia anaonekana kama mtu anayekula wakati wengine hawali chochote. Tunaona kuwa Padri ana chakula wakati wengine hawana. Chakula hapa tunaona kinawakilisha uwezo wa kifedha na mali. Pengine mwandishi alikusudia kumtumia mhusika Padri kuonesha utajiri unaomilikiwa na viongozi wa Kanisa Katoliki. Ni ukweli usiopingika kwamba, katika hali halisi mapadri katika jamii ni watu wenye uwezo wa kifedha. Mapadri walio wengi wanatembelea magari mazuri ya kifahari, wamejenga majumba mazuri nyumbani kwa wazazi wao n.k. Waumini wa kawaida wanaweza kuwa maskini kiasi cha kukosa chakula lakini si mapadri. Tuonavyo sisi,

neno kula limetumika kifasihi na linawakilisha uwezo au utajiri unaomilikiwa na Kanisa Katoliki. Kanisa Katoliki limejikusanyia utajiri mwingi kwa karne nyingi na kwa njia mbalimbali. Kwa mfano makao makuu ya Kanisa Katoliki (*Vatcan*) ni Serikali inayojitegemea.

Aidha, Padri anajitokeza kama mwelekezaji (mwonyesha njia). Hata hivyo tunaona kuwa Padri haijui vyema hiyo njia anayowaelekeza wengine kutokana na matendo yake ya uzinzi, ulevi na tabia ya kukata tamaa. Padri anakunywa pombe usiku na mchana katika riwaya ya *Nagona*. Jambo hili linatufanya tuamini kuwa pengine mhusika Padri amechanganyikiwa au labda ana mawazo mengi. Au labda pombe ni badala ya faraja ambayo angeipata katika ndoa.

Katika hali halisi, mapadri wengi huwa ni wanywaji wa pombe kupindukia. Kwa mfano katika Parokia ya Kilema wakati huo nikiwa darasa la tano kulikuwa na Padri mmoja ambaye alipenda sana kunywa Konyagi na kuvuta sigara kupita kiasi. Mlevi hawezi kufanya maamuzi sahihi na hawezi kumwonyesha njia mtu mwingine kwani ama atamdanganya au atampoteza. Tuonavyo sisi pengine ulevi wa Padri unadokeza hali ya kuchanganyikiwa, kukosa mwelekeo na kukata tamaa.

Pia katika *Nagona*, mhusika Padri anaonekana kukosa heshima kwa wazee (mwenye dharau). Pengine hili linatokana na tofauti za kiimani kati ya wazee hao ambao wengi wao wanatajwa kuwa ni wapagani na Padri ambaye ni mkatoliki. Padri anatarajia kupokea kwanza salamu kutoka kwa wazee badala ya yeye kutoa heshima hiyo eti kwa sababu tu yeye ni Padri na kwamba wakristo wanapaswa kumpa

heshima hiyo. Tuonavyo sisi ni kwamba mwandishi anamwona mhusika Padri kama mtu aliye na kiburi kutokana na nafasi yake ya kidini katika jamii.

Mwisho Padri amejitokeza kama binadamu wa kawaidaa. Anakasirika, anashindwa na anatukana n.k. Pengine mwandishi alikusudia kuonesha kuwa Padri ni binadamu wa kawaida kabisa. Mhusika padri anasema, “Samahani! Mimi pia ni binadamu” Kimsingi kwa kupitia matendo ya mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi tunaona kuwa Padri anajitokeza zaidi kama binadamu wa kawaida kabisa. Labda pengine mwandishi anahoji iwapo nafasi aliyopewa Padri katika jamii anaistahili au la.

4.7.2 Tofauti za Uwasilishaji wa mhusika Padri katika Riwaya za Kezilahabi

Katika riwaya teule za Kezilahabi tulizozitumia katika utafiti wetu, tumegundua kuwa mhusika Padri anachorwa kwa namna mbili tofauti. Kwanza, uhusika wa moja kwa moja ambapo mhusika Padri anajitokeza waziwazi na matendo na maneno yake yanaonekana kupitia mhusika Padri mwenyewe. Uhusika wa aina hii umejitokeza katika riwaya mbili za mwanzo za Kezilahabi yaani, *Rosa Mistika* (1971) na *Gamba la Nyoka* (1979). Uwasilishaji wa aina hii wa mhusika tuonavyo sisi ni rahisi zaidi kwani unatuwezesha kuyaona matendo kutoka kwa mhusika mwenyewe.

Pili, kuna uhusika usio wa moja kwa moja ambapo mhusika Padri anachorwa kupitia nafsi ya msimulizi. Uwasilishaji wa mhusika kwa njia hii umejitokeza katika riwaya ya *Nagona* (1990) ambapo matendo, mwenendo na maneno ya mhusika Padri yanawasilishwa kupitia nafsi ya msimulizi “Mimi”. Uwasilishaji wa aina hii

tuonavyo sisi unaleta ugumu katika kuamua iwapo kuna ukweli kuhusu yale ambayo yanasimuliwa kumhusu mhusika kwani matendo hayaonekani wazi kupitia mhusika mwenyewe. Hata hivyo, namna hizi mbili za kumwasilisha mhusika yule yule mmoja zinakamilishana katika kutupatia picha halisi ya jinsi mhusika Padri alivyo katika riwaya za Kezilahabi na jinsi anavyoonekana katika jamii.

4.7.3 Dhamira Zinazowasilishwa na Mhusika Padri

Swali la pili katika utafiti wetu lilitaka kujua ni dhamira zipi zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya teule?

Katika riwaya za Kezilahabi tulizozitumia katika utafiti wetu, tumejadili dhamira anuai zinazowasilishwa kupitia mhusika Padri katika riwaya hizo. Dhamira hizo ni suala la malezi ya kiroho, unafiki wa viongozi wa Kanisa Katoliki, uonevu na kukosekana kwa haki, na suala la uwezo wa Padri kuondoa dhambi. Tunazijadili dhamira hizo moja baada ya nyingine hapa chini.

4.7.3.1 Dhamira ya Malezi ya Kiroho

Dhamira ya malezi ya kiroho imejitokeza zaidi katika riwaya ya *Rasa Mistika* kupitia kwa mhusika Padri. Tunamwona Padri akitumwa kwenda kumwonyesha mhusika Rosa njia ya wokovu. Hata hivyo, jambo la kushangaza tunaona kuwa malezi haya yanagonga ukuta kwani hayapokelewi na mhusika Rosa. Jambo hili linaashiria kuwa mhusika Padri ameshindwa kutoa malezi ya kiroho yanayostahili. Kwa upande mwingine pia tunaona mwandishi ana lengo la kuonesha kuwa malezi hayo ya kiroho yanayotolewa na mhusika Padri hayana umuhimu wowote. Vyovyote iwavyo, Padri ameshindwa kumlea kiroho Rosa na hili ndilo jambo muhimu zaidi

kwetu. Tulichokibaini katika utafiti wetu ni kuwa Padri ameshindwa kutokana na kukata tamaa. Kushindwa huku, tuonavyo sisi, kunaashiria pia kushindwa kwa mfumo wa dini anaouwakilisha mhusika Padri.

4.7.3.2 Dhamira ya Unafiki wa Viongozi wa Kanisa Katoliki

Wamitila (1982:84) anasema, "*Gamba la Nyoka* inaendeleza unafiki mkubwa ulioenea katika Ukristo kupitia mhusika Padri Madevu na mmoja wa wafuasi wake waaminifu, Mama Tinda." Anaendelea kudai kuwa, mwandishi anagusia uanafiki wa kidini (tafsiri yetu). Wazo hili la Wamitila kama tulivyoona katika tatizo la utafiti ndilo lililotoa mwanga na hamu ya kumchunguza mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Kwa upande mmoja, tunakubaliana na Wamitila kwamba mwandishi anazungumzia suala la unafiki. Hata hivyo tuonavyo sisi unafiki huo si wa Ukristo bali ni wa viongozi wa Kanisa Katoliki. Tunalisema hili kwa sababu zifuatazo:

Kwanza, Padri ni kiongozi wa Kanisa Katoliki na si Kiongozi wa Ukristo wote. Pili, mwandishi alisoma katika Seminari ya Kikatoliki huko Nyegezi Mwanza tangu darasa la tano. Hii ni kwa mujibu wa mahojiano tuliyofanya na mwandishi Mei, 24, 2013. Hivyo, ni dhahiri kuwa mwandishi alikuwa karibu na mapadri waliokuwapo seminarini hapo kwa muda mrefu. Pengine tunaweza pia kusema kuwa huenda tabia anazozijadili kupitia mhusika Padri katika riwaya zake aliziona kwa mapadri hao ambao alihusiana nao wakati wa maisha yake ya seminarini.

Swali muhimu ambalo tunapaswa kujiuliza ni je, ni kwa kiasi gani maisha ya mhusika Padri, maamuzi yake na matendo yake yanatokana na kazi yake kama Padri

wa Kikatoliki? Nini haswa kinachotawala maamuzi ya mhusika Padri? Je, ni utashi binafsi au pengine anabanwa na mazingira yanayomzunguka? Je, viongozi walioko juu ya Padri ni kwa kiasi gani wana mchango katika maisha ya kinafiki ya mhusika Padri? Je, sheria ya Padri kutokuoa aliitunga Padri au inatokana na viongozi waliotangulia katika dini hiyo?

Kimsingi iwapo tutaweza kuyajibu maswali yote haya, tutaweza kubaini kuwa mhusika Padri ni kiwakilishi tu cha mfumo wa kinafiki wa dini ambao haukuanzishwa na Padri bali na wale waliotangulia katika Kanisa Katoliki. Pengine tunaweza kujiuliza swali: ni kwa nini mapadri hawaoi? Ni amri ya Mungu au ni katazo la dhehebu Katoliki? Je, Biblia ambacho ndicho kitabu kinachotumiwa na Kanisa Katoliki na madhehebu mengine inasemaje kuhusu suala la kuoa?

Maandiko ya Biblia, yanatuonesha kuwa Mtume Petro ambaye anachukuliwa na Wakatoliki kuwa Papa wa kwanza wa dini hiyo alikuwa ameoa. Hili tunaliona katika vitabu vya Injili ya Mtakatifu Mathayo, Injili ya Mtakatifu Marko, na Injili ya Mtakatifu Luka; kwa kutaja tu sehemu chache. Kwa mfano katika *Mathayo 8:14-15*, Biblia inasema,

> "Hata Yesu alipofika nyumbani kwa Petro, akamwona mkwe wa Petro, mamaye mkewe, amelala kitandani hawezi homa. Akamgusa mkono, homa ikamwacha;.."

Maneno yanaoyofanana na hayo yanapatikana pia katika *Marko 1:30*, ambapo Biblia inasema,

> "Naye mkwewe Simoni, mamaye mkewe, alikuwa kitandani, hawezi homa; na mara wakamwambia habari zake."

Maneno mengine yanapatikana katika *Luka 4:38*, Biblia inasema,

> "Akatoka katika Sinagogi akaingia katika nyumba ya Simoni. Naye mkwewe Simoni, mamaye mkewe, alikuwa ameshikwa na homa kali, wakamwomba kwa ajili yake."

Maandiko haya yanaonesha kuwa anayeaminiwa kuwa papa wa kwanza wa Kanisa Katoliki (kama kweli ndiye) alikuwa ameoa. Simoni ni jina jingine la mtume Petro. Ikumbukwe kwamba Kanisa Katoliki hufundisha kwamba Petro ni mwamba ambao Yesu alisema atalijenga kanisa lake. Kama Petro alikuwa ameoa kitendo cha mapadri kutokuoa lakini wanafanya zinaa ni uasi dhidi ya Kiongozi wao. Tuonavyo sisi, kama mapadri wangeruhusiwa kuoa kama ilivyokuwa mwanzo huenda tatizo la kashfa za ngono, ushoga na ulawiti ambazo zimekuwa zikilikumba kanisa hilo kwa muda mrefu zingepungua. Ndio maana kwa kulijua hili Biblia yenye vitabu vya Deuterekanoni inayotumiwa na Wakatoliki inasema,

> "Hata hivyo, kama mtu hawezi kujizuia, basi na aoe; maana ni afadhali zaidi kuoa kuliko kuwaka tamaa." (1Wakorintho 7:9)

Si kusudi la utafiti huu kueleza au kuuaminisha umma kuwa pengine waliooa au Wachungaji wa makanisa mengine ambao huoa hawawezi kuzini. Tuonavyo sisi, kitendo cha mapadri kutokuoa ni kuuambia umma kuwa wao ni watu waliotengwa na walio karibu zaidi na Mungu na hawana kiu ya tendo la ngono ilihali mambo ni kinyume chake kama inavyoonekana katika *Gamba la Nyoka*. Ingawa kuna hoja kwamba Yesu hakuoa, bado tutabaki na swali la kwa nini Yesu alimchagua Petro aliyekuwa ameoa kuwa kiongozi wa kwanza wa kanisa? Tuonavyo sisi, Yesu hakuwa na muda mrefu wa kuishi duniani, hivyo hakuona umuhimu wa kuoa na kuzaa watoto ambao angewaacha baada ya miaka mitatu. Ndio maana suala la kuoa

au kutokuoa linapaswa kuwa uamuzi wa hiari wa mtu na si sheria ya dhehebu fulani la dini.

Huu ndio unafiki wa viongozi wa Kanisa Katoliki unaojitokeza katika kazi za Kezilahabi. Swali ni je, unafiki huu ni kweli na halisi katika jamii zetu au sio? Uzoefu wa kijamii wa matukio mbalimbali yanayowahusisha mapadri unaonesha kuwa tabia hii ya unafiki wa mapadri ni wazi na imekithiri. Mapadri wamekuwa wakituhumiwa kwa matukio mbalimbali ya kingono. Mfano dhahiri na halisi ni wa tukio la Padri aliyefumaniwa na mke wa mtu. Tukio hili limeandikwa katika gazeti la *Risasi* la tarehe 4-7, Mei, 2013.

Kumbe basi unafiki unaojitokeza katika *Rosa Mistika* (wa kufundisha lakini kutoishi mafundisho hayo) na katika *Gamba la Nyoka* (kujifanya kutokuoa lakini kufanya uzinzi) ni dhahiri na halisi katika jamii zetu hata sasa.[1] Huu ni ushahidi kuwa mambo mengi yanayojadiliwa na Kezilahabi kupitia mhusika Padri katika riwaya zake ni mambo halisi katika jamii zetu. Kezilahabi amethubutu kuufunua unafiki wa hali ya juu uliojificha ndani ya mfumo wa dini Katoliki kupitia kwa mhusika Padri.

[1] Kwa mfano, mnamo mwaka 1995, dada yetu aliyekuwa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Kisomachi inayomilikiwa na kanisa Katoliki, alionekana ana ujauzito. Alihojiwa sana ili amtaje mwanamume aliyempa ujauzito huo bila mafanikio yoyote. Hatimaye iligundulika kupitia dada yetu mwingine (mtoto wa mama mkubwa aliyekuwa karibu sana na dada yetu wakisoma shule moja) kuwa aliyekuwa amempa dada yetu ujauzito huo ni Padri aliyekuwa rafiki wa karibu sana wa mjomba ambaye dada alikuwa akiishi kwake na ndiye aliyekuwa anamsomesha. Jambo hili nililithibitisha mwenyewe siku moja nilipomtembelea mama mdogo mahali ambako dada yetu alikimbilia baada ya kufukuzwa kwa mjomba. Nikiwa hapo asubuhi moja nilishuhudia gari ikifika na kusimama na akateremka mwanamume ambaye nilimtambua kuwa Padri kutokana na alama ya kimsalaba aliyokuwa ameivaa katika kola ya mavazi yake ya kiraia. Aliniuliza dada (alimtaja jina) yuko wapi nikamjibu yuko ndani na alimfuata huko. Baada ya miezi michache dada yetu alijifungua mtoto lakini kwa bahati mbaya yule mtoto ilidaiwa kwamba alifariki. Hapa tunaweza kujiuliza swali: Je, yule mtoto alifariki kwa mpango wa Mungu au labda kulikuwa na njama za kupoteza ushahidi? Swali hili linaweza kujibiwa na marehemu kwa kuwa ni yeye peke yake tu anaweza kutuambia ukweli.

4.7.3.3 Dhamira ya Uonevu na Kukosekana kwa Haki

Dhamira ya uonevu na kukosekana kwa haki ni suala mojawapo linalojadiliwa na Kezilahabi kupitia mhusika Padri. Dhamira hii tunaiona kutokana na yale yaliyowakumba vijana wawili, Mamboleo na Mambosasa kupitia mhusika Padri Madevu. Je, ni kweli kuwa kupitia Padri uonevu na kukosekana kwa haki vinaweza kutokea? Kulijibu swali hili tujiulize, je, ilikuwa haki kwa Mambosasa na Mamboleo kuhukumiwa pasipo hata kupewa nafasi ya kusikilizwa na kujitetea? Pengine hali hii inaonesha kuwa mapadri kwa sababu ya hadhi yao hupewa upendeleo wasiostahili katika jamii? Hali halisi katika jamii ikoje? Kwa mfano, katika mabenki, mahakama, mahospitali, na kadhalika? Katika hali halisi mapadri na hata viongozi wengine wa kanisa huwa wanapewa upendeleo hata pale ambapo hawastahili/si haki yao. Kwa mfano, huwezi kumkuta Padri mahali kama vile benki amesimama akisubiri huduma. Nimewahi kushuhudia hali kama hii ambapo siku moja nikiwa napata huduma katika benki moja, alikuja Padri mmoja ninayemfahamu na kuingia moja kwa moja katika chumba kimojawapo cha benki ambako alikwenda kupatiwa huduma akituacha wote tuliokuwa tumepanga foleni tukisubiri huduma.

Hivyo, suala la uonevu na ukosefu wa haki linaloshughulikiwa na Kezilahabi kupitia mhusika Padri, liko katika jamii hata leo kwa namna moja au nyingine.

4.7.3.4 Dhamira ya Uwezo wa Padri Kuondoa Dhambi

Suala la uwezo wa Padri kuondoa dhambi limeshughulikiwa katika *Gamba la Nyoka* na *Nagona*. Tunaweza kujiuliza swali: je, ni kweli Padri anao uwezo wa kuondoa dhambi? Hili ndilo swali ambalo linamtatiza Kezilahabi. Tatizo liko wapi? Mwandishi anaonesha kuwa Padri ni mtenda dhambi. Hili linaondoa uwezo wa Padri

kuondoa dhambi kwani yeye mwenyewe ni mwanadamu wa kawaida na ambaye anashiriki katika kutenda dhambi zilezile ambazo waumini walioko chini yake wanaziungama kwake. Kwa mfano, katika *Gamba la Nyoka*, tunamwona Padri Madevu anafanya zinaa na Mama Tinda na wanaporudi sebuleni Mama Tinda anapiga magoti na kuomba baraka kutoka mshirika mwenzake katika dhambi ya uzinzi (Padri Madevu). Hiki ni kichekesho na kejeli ya hali ya juu sana. Pengine tunaweza kujiuliza swali: Je, yawezekana yeye aliye mchafu kumfundisha au kumfanya mchafu kuwa msafi? Je, mwalimu aweza kufundisha kitu ambacho yeye mwenyewe hakijui? Kimsingi aliye mchafu kamwe hawezi kumfundisha mwingine jinsi ya kuwa msafi. Anachoweza kufundisha aliye mchafu ni jinsi ya kuwa mchafu na kinyume chake ni uongo na unafiki wa hali ya juu.

4.7.4 Motifu ya Padri Aliyeshindwa

Swali la tatu katika utafiti wetu lilikuwa linauliza iwapo kuna motifu yoyote inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya teule. Tumejadili na kuona kuwa motifu ya Padri aliyeshindwa inajitokeza katika riwaya za Kezilahabi tulizozishughulikia katika utafiti wetu. Hitimisho hili limefikiwa kwa kuchunguza uradidi wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi, na uradidi na/au uhusiano wa dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Tunaweza kujiuliza swali; Je, kwanini mhusika Padri?

Katika mahojiano na mwandishi Mei, 24, 2013, aliulizwa ni kwa nini mhusika Padri amejitokeza zaidi ya mara tatu katika kazi zake na iwapo kuna jambo lolote alilotaka kusisitiza kupitia mhusika huyo. Katika kulijibu swali hili, mwandishi alisema kuwa

mhusika Padri ametokea hasa kwa mambo ya kiroho, kuleta mgongano uliopo kati ya maisha ya kawaida na yale ya kiroho.

Kimsingi, ukweli huu unajitokeza katika kazi za Kezilahabi. Tunaona mhusika Padri anavutwa pande mbili, anataka kuwa Padri na wakati huohuo anataka kuwa mwanamume wa kawaida na kufaidi matunda ya ndoa. Jambo hili ndilo lililotufanya tuone kuwa mhusika Padri anadokeza motifu ya Padri aliyeshindwa. Ipo methali ya Kiswahili isemayo: Mshika mbili, moja humponyoka na Mtaka yote, hukosa yote! Hiki ndicho kinachotokea kwa Padri, na matokeo yake yanakuwa kushindwa kusimamia kauli na mafundisho yake na kukosa maadili. Pengine tunaweza kujiuliza swali: Nini umuhimu wa aliyeshindwa katika jamii? Mara nyingi katika jamii zetu watu hupenda kuwataja na hata kuhusiana na wale walioshinda.

Tunaweza kujiuliza swali, motifu ya Padri aliyeshindwa inaashiria nini? Tuonavyo sisi mhusika Padri hakujitokeza tu kibahati katika riwaya za Kezilahabi tulizozichunguza, hivyo basi, motifu ya Padri aliyeshindwa inaashiria kushindwa kwa Padri, kwanza, kama mwanamume mwenye maamuzi na utashi binafsi, na kama kiongozi wa dini. Kwa upande mwingine, tunaona kuwa motifu ya Padri aliyeshindwa inaashiria kushindwa kimaadili kwa viongozi wa dini katika mfumo wa dini anaouwakilisha mhusika Padri.

4.8 Ufaafu wa Nadharia ya Uhalisia wa Kimarx Tuliyoitumia

Je, nadharia ya uhalisia wa Kimarx imetusaidiaje? Katika utafiti wetu tumeona kuwa matendo mengi yanayofanywa na mhusika Padri ni halisi. Ni matukio ya kuaminika

ambayo tunaweza kukutana nayo katika jamii zetu. Hivi ndivyo inavyotaka nadharia ya uhalisia. Nadharia ya Uhalisia wa Kimarx imetuwezesha kuhusisha matendo ya mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi, na matendo yanayofanywa na Padri halisi katika jamii. Tumeona kuwa upo uhusiano mkubwa sana kati ya matendo ya mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi na matendo yanayofanywa na mapadri halisi katika jamii zetu. Matendo kama vile uzinzi, ulevi, kuongoza ibada, n.k. ni matendo ambayo hufanywa na mapadri katika jamii zetu siku kwa siku. Kumbe basi, yale yanayosemwa kumhusu mhusika Padri Madevu katika *Gamba la Nyoka* (1979), miaka 34 iliyopita, yapo katika jamii zetu na yanafanywa na mapadri hata leo. Rejea tukio la Padri aliyefumaniwa na mke wa mtu lililoripotiwa katika gazeti la *Risasi* la Jumamosi, Mei, 4-7, 2013. Kwa ujumla, yapo matukio mengi ambayo yamekuwa yakiripotiwa kuhusu kashfa za ngono kwa mapadri wa Kanisa Katoliki hapa Tanzania na kwingineko. Hata katika *Nagona*, riwaya ambayo ni ya kifalsafa zaidi, tunaweza kuona uhalisia kwa kumzingatia mhusika Padri mwenye tabia ya ulevi.

4.9 Hitimisho

Katika sura hii tumechambua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti na tumefanya mjadala juu ya matokeo ya utafiti. Tumeona uhusika wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi unavyoweza kuchambuliwa, ambapo tumemwona mhusika Padri kama kiongozi wa Kanisa katika jamii, Padri kama mlezi wa kiroho, Padri kama mwanamume wa kawaida katika jamii, Padri kama mtu mwenye sauti katika jamii, Padri kama mtu mwenye uwezo kuliko wengine katika jamii, Padri kama mwelekezaji (mwonyesha njia), Padri kama mlevi, Padri kama mtu asiye na heshima kwa wazee na Padri kama binadamu wa kawaida. Pia tumeangalia dhamira

zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi ambazo ni: suala la malezi ya kiroho, unafiki wa viongozi wa Kanisa Katoliki, uonevu na kukosekana kwa haki, na suala la uwezo wa Padri kuondoa dhambi. Aidha, tumejadili motifu inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi ambapo tumegundua kuwa motifu ya Padri aliyeshindwa inajitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Pia tumeona kuwa mhusika Padri kutokana na uradidi wake na dhamira anazoziwasilisha, ni mhusika wa kimotifu (mhusika anayewakilisha motifu) katika riwaya za Kezilahabi. Tumejenga mjadala juu ya matokeo ya utafiti na mwisho tumejadili juu ya ufaafu wa nadharia ya uhalisia wa Kimarx tuliyoitumia katika utafiti wetu.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inahitimisha utafiti unaohusu usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona (*1990). Sura hii imegawanywa katika sehemu tano: Sehemu ya kwanza ni utangulizi wa sura hii, sehemu ya pili inahusu muhtasari wa utafiti, sehemu ya tatu inaeleza matokeo ya utafiti, sehemu ya nne inaeleza mchango wa utafiti, na sehemu ya tano inahusu mapendekezo ya tafiti zijazo.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu tulioufanya ulilenga kuchunguza suala la usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990). Utafiti huu ulijikita hasa katika kuchunguza mambo makuu matatu; kwanza, kuchambua uhusika wa mhusika Padri katika riwaya teule, pili, kujadili dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya teule, na tatu, kubainisha motifu inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya teule. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia wa Kimarx katika kuhusisha matendo ya mhusika Padri katika riwaya teule za Kezilahabi, na matendo ya Padri halisi katika jamii.

Tasinifu hii imeundwa na sura tano: Katika sura ya kwanza tumejenga msingi wa tasinifu hii kwa kutoa usuli wa tatizo la utafiti. Tumeeleza malengo, maswali ya

utafiti, umuhimu wa utafiti na mawanda ya utafiti. Sura ya pili imejengwa kwa mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusiana na utafiti wetu pamoja na kiunzi cha nadharia kwa lengo la kusaidia kujenga hoja ya umuhimu wa utafiti huu. Mambo yanayoijenga sura ya tatu ni mbinu za utafiti zikijumuisha mbinu za ukusanyaji data, sampuli na usampulishaji, uchambuzi, uchakataji na uwasilishaji wa data, vifaa vya utafiti na eneo la utafiti. Kiini cha sura ya nne katika utafiti huu ni uchambuzi wa data, matokeo ya utafiti na mjadala. Ni katika sura hii ambapo uhusika wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi umeelezwa katika sura zake mbalimbali, dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi zimejadiliwa, motifu ya Padri aliyeshindwa inayojitokeza katika riwaya teule za Kezilahabi imebainishwa na mjadala juu ya matokeo ya utafiti umefanywa.

Aidha, mjadala unajengwa juu ya uhusika wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Pia mjadala unajengwa juu ya tofauti za uwasilishaji wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi, mjadala unajengwa juu ya dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi zilizochunguzwa pamoja na mjadala juu ya motifu ya Padri aliyeshindwa inayojitokeza katika riwaya teule za Kezilahabi kupitia mhusika Padri. Mwisho ufaafu wa Nadharia ya Uhalisia wa Kimarx katika utafiti wetu umejadiliwa. Sura ya tano na ya mwisho katika utafiti wetu ni ya matokeo ya utafiti, ugunduzi, mchango na mapendekezo ya tafiti zijazo.

5.3 Matokeo ya Utafiti na Ugunduzi

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona*

(1990). Utafiti huu pia uliongozwa na malengo matatu mahususi ambayo ni kuchambua uhusika wa mhusika Padri katika riwaya teule, kujadili dhamira zinazowasilishwa kupitia mhusika Padri katika riwaya teule na kubainisha motifu inayojitokeza kupitia mhusika Padri katika riwaya teule.

Kwa kumtumia mhusika Padri katika riwaya teule, mtafiti alifuatilia hatua kwa hatua matendo yake, maneno yake na yale ambayo wengine wanasema kumhusu, na vile mwandishi alivyomwelezea. Kupitia mambo haya tumeweza kugundua kuwa mhusika Padri anasawiriwa katika nafasi mbalimbali kama vile: Padri kama kiongozi wa Kanisa katika jamii ambapo ana jukumu la malezi ya kiroho na kufanya shughuli za ibada, Padri kama mwanamume wa kawaida katika jamii ambapo anaonekana katika matendo kama vile uzinzi, ulevi, ugomvi na kadhaliaka. Pia tumeona kuwa mhusika Padri anatokea kama mtu mwenye sauti katika jamii, kama mtu mwenye uwezo kuliko wengine, na kama mwelekezaji.

Pia tumegundua kuwa mhusika Padri katika riwaya teule za Kezilahabi anawasilisha dhamira kuu nne ambazo ni suala la malezi ya kiroho, unafiki wa viongozi wa kanisa Katoliki, uonevu na kukosekana haki na suala la uwezo wa Padri kuondoa dhambi. Kwa kutumia nadharia ya Uhalisia wa Kimarx tumeona kwa mifano mbalimbali kwamba matendo yanayojadiliwa katika riwaya za Kezilahabi kupitia kwa mhusika Padri ni halisi katika jamii.

Aidha tumegundua pia kwamba motifu ya Padri aliyeshindwa inajitokeza katika riwaya teule za Kezilahabi. Hii ni aina mpya ya motifu katika fasihi ya Kiswahili.

Tumeweza pia kugundua kuwa mhusika Padri si mhusika wa kawaida bali ni mhusika wa kimotifu kutokana na uradidi wake na kwa sababu ya uradidi na/au uhusiano wa dhamira zinazowasilishwa na mhusika Padri katika riwaya teule ambazo zote zinaonesha hali ya kushindwa kwa mhusika Padri.

5.4 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu ni muhimu katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili, hususan riwaya ya Kiswahili na hasa katika kumwelewa mhusika Padri anayejitokeza mara nyingi katika riwaya za Kezilahabi, kwa kutumia nadharia ya uhalisia wa Kimarx, ili kueleza iwapo yale yanayoelezewa kupitia mhusika Padri ni halisi katika jamii.

Pia utafiti huu umeongeza aina za wahusika katika fasihi ya Kiswahili na pia umebainisha vigezo vya kumtambua na kumfasili mhusika wa kimotifu. Vigezo hivyo ni uradidi wa mhusika huyo katika kazi zaidi ya mbili za mwandishi mmoja na uradidi na /au uhusiano wa dhamira zinazowasilishwa na mhusika huyo katika kazi hizo.

Aidha utafiti huu umeweka msingi kwa tafiti za kinadharia zitakazomchambua mhusika Padri katika fasihi ya Kiswahili na nyanja nyingine za fasihi ya Kiswahili. Huu ni utafiti wa kwanza wa kinadharia kuchambua usawiri wa mhusika Padri katika fasihi ya Kiswahili hususan, riwaya za Kezilahabi.

5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Utafiti uliofanywa ulilenga kuchunguza usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990). Katika utafiti huu tuligundua mambo mbalimbali ambayo tunapendekeza watafiti wengine wayafanyie kazi. Utafiti huu unapendekeza utafiti zaidi ufanyike juu ya kipengele cha mhusika wa kimotifu katika fasihi ya Kiswahili.

Pia tunapendekeza kwamba utafiti ufanyike juu ya motifu ya Padri aliyeshindwa ili kuona kama inajitokeza pia katika tanzu nyingine za fasihi andishi ya Kiswahili kama vile tamthiliya ya Kiswahili na ushairi

Aidha, utafiti huu unapendekeza uchunguzi zaidi ufanyike juu ya mhusika Padri katika fasihi ya Kiswahili hususan riwaya ya Kiswahili kwa kutumia mkabala linganishi ili kubaini iwapo upo mfanano kati ya mwandishi mmoja na mwingine katika kumchora mhusika Padri au iwapo ziko tofauti na kwa nini.

MAREJELEO

Chaligha, E. N. (2011). "Usawiri wa Mwanamke na Mgawanyo wa Majukumu Kijinsia katika Fasihi: Picha ya Katuni Mnato za Kiswahili." Tasnifu ya M.A, Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Septemba 2011

Chama cha Biblia (1997). *BIBLIA: Maandiko Matakatifu*, Nairobi na Dodoma: Chama cha Biblia cha Kenya na Chama cha Biblia cha Tanzania

_____ (2001), *BIBLIA HABARI NJEMA KWA WATU WOTE: Yenye Vitabu vya Deuterekanoni*,(Toleo la Pili), Nairobi na Dodoma: Chama cha Biblia cha Kenya na Chama cha Biblia cha Tanzania Diegner, L. (2002) "Allegories in Euphrase Kezilahabi's Early Novels" AAP *Swahili Forum IX*, 72, pp 43-74

Gibbe, A.G. (1982) " Baadhi ya Taswira katika *Gamba la Nyoka*" *Kiswahili*, Juzuu 49, uk 9-14

Gromov, M. D. (1998) "Nagona and Mzingile- Novel, Tale or Parable? AAP 55 *Swahili Forum V*, pp 73-78

Kanwa, O. (2011). "Usawiri wa Wahusika wa Kiume katika Riwaya za Kiswahili __ Mkabala Linganishi." Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Septemba, 2011

Kezilahabi, E. (1971) *Rosa Mistika*, Dar es Salaam: East African Literature Bureau
_____ (1979). *Gamba la Nyoka*. Arusha: East Africa Publications

_____ (1990, 2011). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press, Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited

Kothari, C. R. (2004) *Research Methodology: Methods and Techniques* (Second Revised Edition), New Delhi: New Age International Publishers

Lyatuu, L. (2011). "Usawiri wa Wahusika Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na wa Kiume _ Uchunguzi katika Riwaya Teule," Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Septemba 2011

Madumulla, J. S. (1987) "Maendeleo ya Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili Tanzania" *Kiswahili*, Juzuu 54/1&54/2, uk 66-76

_____(2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Nairobi: Phoenix Publishers

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi,* Nairobi: East African Educational Publishers

Mukama, S. (2011). "Usawiri wa Wahusika Walemavu katika Fasihi ya Kiswahili," Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Septemba 2011

Mulokozi, M.M. (1983) "*Dunia Uwanja wa Fujo*" *Kiswahili,* Toleo 50/1, uk 1-12

Mbatiah, M. (1998) "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*" *Mulika* Na 24, uk 1-13

Mlacha, S.A.K. (1985) "Wahusika katika Riwaya za Kiswahili Tanzania 1970-1982," *Mulika* Na 27, uk 29-45

_____ (1986) "The Identification of Personality Differences in Kiswahili Prose Fiction" *Kiswahili,* Juzuu 53/1 & 53/2, uk 146-167

_____ (1987) "Aggression as a Mental and Social Disorder: A Study of Swahili Novels" *Kiswahili,* Juzuu 54/1 & 54/2, uk 77-91

_____ (1991) "Point of View as a Stylistic Device in Kiswahili Novels" Kiswahili, Juzuu 58, uk 54

Msokile, M. (1992), *Misingi ya Hadithi Fupi*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press

Mwangoka, N. (2011). "Motifu za Safari na Msako katika Makuzi ya Wahusika wa Riwaya za E. Kezilahabi," Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Septemba 2011

Njogu, K. & R, Chimerah, (2008)(Toleo la Pili). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu,* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Ntarangwi, M. (2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Rock Island, IL 61201: Augustana College

Oxford na TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la Pili),* Nairobi na Dar es Salaam: Oxford University Press, East Africa, Ltd na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Senkoro, F. E. M. K. (1976) "Utamaduni katika Riwaya ya Kiswahili" *Kiswahili,* Tol 46/2, uk 74-94

_____(2011)(Toleo la Pili).*Fasihi,* Dar es Salaam: KAUTTU Limited

Wamitila, K. W.(1991) "*Nagona* and *Mzingile*: Kezilahabi's Metaphysics,"*Kiswahili* Jz 58 uk 62-67

_____ (1998)"A Philosophical Labyrinth: Tracing Critical Motifs in Kezilahabi's Prose Works AAP 55: *Swahili Forum V*, pp 79-91

_____(2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake,* Nairobi: Phoenix Publishers Limited

_____(2003) "Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi's *Nagona* and *Mzingile* and Juan Ruflo's *Pedro Peramo*" *Kiswahili,* Juzuu 66, uk 49-58

Kutoka Mtandaoni

Arachne Jericho (2012) http://spontaneousderivation.com/2012/11/13/writing-dissonance-disecting-the-independent-character. imesomwa Januari 7,2013

www.en.wikipedia.org/wiki/motif. imeboreshwa Januari 15,2013. Imesomwa terehe 06/05/2013

VIAMBATANISHO

Kiambatisho 1: Mwongozo wa Mahojiano na Mwandishi E. Kezilahabi

1. Ni jambo gani lililokusukuma kuiandika riwaya ya *Rosa Mistika*?

.....

.....

.....

.....

.....

.....

2. (a) Je, uliwahi kusoma seminari?

.....

.....

.....

(b). Unaweza kutueleza kwa kifupi maisha yako ya seminari yalikuwaje?

.....

.....

.....

.....

(c) Je, uliyapenda maisha ya seminari au uliyachukia?

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3. Je, ungependa kuwa Padri? Kama ndio kwa nini? Na kama hapana kwa nini?

.....

.....

.....

.....

4. Mhusika Padri amejitokeza zaidi ya mara tatu katika riwaya zako. Je, kuna jambo lolote unalotaka kusisitiza kupitia mhusika huyo?

.....

.....

.....

5. Ni dhamira zipi ambazo ulikusudia kuwasilisha kwa jamii kupitia mhusika Padri katika riwaya zako? Taja angalao nne.

(i).....

(ii).....

(iii).....

(iv).....

6. Katika *Rosa Mistika* mhusika padre anatumwa kumshauri Rosa lakini ushauri wake unapuuzwa na Rosa. Je, ulikusudia kuonesha kushindwa kwa mhusika Padri au kutokutii kwa Rosa au uhuru wa utashi binafsi?

.....

.....

.....

.....

7. Katika *Gamba la Nyoka* wahusika wawili mapadri wote ni wazinzi. Je, ulikusudia kuonesha unafiki wa Ukristo au unafiki wa viongozi wa kanisa?

.....

.....

.....

8. Ingawa Padri ni miongoni mwa wahusika wachache walio na sauti katika *Nagona*, mhusika huyu pia ni mlevi. Ulikusudia kuiambia nini jamii?

.....

.....

.....

9. Je, ni sahihi tukisema kuwa mhusika Padri katika kazi zako ni mhusika wa kimotifu kutokana na uradidi wake?

.....

.....

.....

.....

.....

.....

10. Je, katika maisha yako ya awali ya seminari uliwahi kukutana kihalisi na mapadri wenye tabia zinazojitokeza katika riwaya zako au pengine kusimuliwa na rafiki zako kuwahusu?

.....

.....

.....

11. Je, unadhani kuwa lengo lako kwa kumtumia mhusika Padri katika riwaya zako limetimia au la?

.....

.....

.....

.....

.....

12. Je, nini matarajio yako ya baadaye katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili?

.....

.....

.....

.....

.....

ASANTE SANA KWA USHIRIKIANO WAKO!

Kiambatisho 2: Picha ya Kezilahabi

Picha kwa mujibu wa www.jahhn-bibliothek.ifeas.uni mainz.de/Bilder_allgemein/Kezilahabi-019_16.JPG.